# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumanne Machi 9, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580514

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.co... www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



Nipashe **TESA**

Jumanne Machi 9, 2021

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

Jasiri mwenye ulemavu wa kuona anayemudu mzigo mzito maishani

UN yaitaka dunia ione mwisho wa enzi nishati gesi, makaa ya mawe

TEKNOLOJIA

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

Kuchafuliwa na tuhuma za uzushi vyazamisha baharini jahazi 50/50

**Sababu** kupungua kwa mfumuko wa bei hizi

UKURASA 2



**Mama** Mwinyi ataka vita dhidi ya udhalilishaji

UKURASA 3

UKURASA 11

# Wataalamu watafiti chanjo corona nchini

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**SHULE ZAFUNGIWA KULAZA WANAFUNZI**

SHULE mbili za msingi ambazo ni Kido na Talent wilayani Kyerwa mkoani Kagera, zimefungiwa...

UKURASA WA 8

**UPELELEZI KESI YA MWIJAKU WAIVA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imeambiwa kwamba upelelezi wa kesi...


## TAKUKURU yataja vishawishi rushwa ya ngono vyuoni

UKURASA 3




Wanawake wakicheza katika viwanja vya Mlimani City jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

## Tanzania yajivunia mafanikio ya utekelezaji maazimio ya Beijing

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** NDAYIRAGIJE, MAXIME KATIKA MIZANI YANGA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Wataalamu watafiti chanjo ya corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema kuwa hivi sasa wataalamu wake wapo katika mchakato wa kufanya utafiti utakaosaidia kupata chanjo ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu (Covid-19).

Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, alisema hayo jana jijini hapa, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali yaliyotekelezwa na serikali.

Akijibu moja ya maswali kuhusu takwimu za wagonjwa wa corona nchini, Dk. Abbas alisema kitendo cha mataifa mengine kulalamikia Tanzania hakina maana kwa kuwa corona ipo kila nchi na hakuna sababu ya kulalamikia nchi nyingine. Alisema kama taifa lina msimamo wake na hakuna mtu wa kuubadilisha.

"Kuna maneno mengi yamekuwa yakiendelea hivi sasa watu wanauliza pia kwanini hatutaki kupatiwa chanjo ya corona kama mataifa mengine, waendelee kuwajaribu wengine na hiyo chanjo sisi pia tupo katika utafiti watu wetu wanafanya utafiti kutafuta chanjo yetu kwani hata miaka ya nyuma tulishawahi kuwa na chanjo yetu wenyewe," alisema.

Dk. Abbas alisema ni ajabu kusikia taifa moja linamlalamikia mtu kuhusu kutoa takwimu za corona wakati na wao pia ni waathirika.

"Ni ajabu taifa moja kumlalamikia mtu mwingine wakati na kwake lipo tatizo kama hilo badala ya kushughulikia tatizo lako unamlalamikia mwingine wao waendelee na majaribio ya chanjo yao kama itathibitishwa tutaangalia namna ya kuitumia, lakini hatutakuwa watu wa kufanyiwa majaribio ya chanjo yao," alisisitiza Dk. Abbas.

Akizungumzia kuhusu mahindi kutoka Tanzania yaliyozuiliwa mpakani mwa Kenya, alisema ni kweli tukio hilo limetokea na serikali inaendelea kufanya mawasiliano kujua tatizo.

"Kweli kuna mahindi yamezuiliwa kuingia nchini Kenya katika mpaka wa Namanga na hili ni suala linalohusisha serikali, lazima pande zote mbili zikae ili kuona shida ipo wapi kwanini katika mpaka wa Hororo yanaingia," alisema.

Dk. Abbas pia alisema kuwa serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria imetoa mwongozo kwa wizara zote kuanza na kukamilisha tafsiri za sheria kuu zote zipatazo 450, kabla ya Desemba mwaka huu. "Napenda kutumia nafasi hii kuujulisha umma kuwa serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Bunge lililopita, imekamilisha na ikapitishwa Muswada na sasa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1 ya mwaka 2021, ambayo pamoja na mambo mengine, imeruhusu rasmi lugha ya Kiswahili kutumika mahakamani, kuwa lugha ya uandishi wa sheria na utoaji haki kwa ujumla," alisema Dk. Abbas.

Alisema wizara hiyo imeshatoa mwongozo kwa wizara zote kuanza na kukamilisha tafsiri za sheria kuu zote zipatazo 450, zinazosimamiwa na wizara husika au taasisi zilizo chini ya wizara hizo.

"Kwa mujibu wa mwongozo huo pia itaandaliwa Kamusi ya Istilahi za Kisheria, tafsiri ya sheria kuu na kamusi vinapaswa kukamilika ifikapo Desemba, 2021 ili kupisha mchakato mwingine muhimu wa kutafsiri kanuni za sheria mbalimbali zinazofikia 15,000 zoezi linalotarajiwa kukamilika ifikapo Juni 2022," alisema.

Alieleza umuhimu wa wizara zote kuzingatia kalenda hiyo, pia wataalamu wa Baraza la Kiswahili nchini (BAKITA) wanatakiwa kushiriki na kushirikishwa katika mchakato wote.

Alisema kila wizara au taasisi inatakiwa kuhakikisha inashirikisha BAKITA kwa kuwa ndiyo wenye lugha yao ya Kiswahili.

Akizungumzia mafanikio ya serikali katika sekta ya elimu, alisema katika kipindi cha miaka sita serikali imefanikiwa kufanya marekebisho makubwa katika sekta hiyo kwa kutoa kiasi cha Sh. trilioni 1.291 fedha ambazo zimewekezwa katika kuwezesha vijana kupata elimu bila malipo kuanzia darasa la awali hadi kidato cha nne.

Akizungumzia elimu ya juu, alisema katika kipindi cha miaka sita serikali imetoa kiasi cha Sh. trilioni 2.82 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa vyuo vikuu nchini.

"Zamani suala la mikopo kwa wanafunzi ndiyo ilikuwa kero kubwa kwa wanafunzi kila wakati ulikua ukisikia migomo na maandamano, lakini hivi sasa 'boom' linafika kwa wakati na kusaidia vijana wetu kuendelea kusoma bila kuwa na shida yoyote," alisema.

Pia miradi ya maji 177, ambayo ilikuwa chechefu serikali iliamua kuichukua na hadi sasa 85 imekamilika na kuanza kutoa maji.




Watumishi wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma wakiwa katika sherehe za Siku ya Wanawake Duniani mjini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tanzania yajivunia utekelezaji maazimio ya Beijing

**Na Elizabeth Zaya**

TANZANIA imejivunia kutekeleza maazimio mengi yaliyofikiwa Beijing miaka 25 iliyopita, huku ikitaja changamoto chache ambazo zimebaki ikiwamo suala la madhila ya unyanyasaji na ukatili ambayo bado yanawakumba wanawake na watoto wa kike.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, wakati akizungumza katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

"Mazimio ya Beijing yalitoa vipaumbele 12, kwa hiyo yapo ambayo tumeyafanya vizuri sana, lakini machache hatujafanya vizuri likiwamo la kumwangalia mtoto wa kike, mwanamke na unyanyasaji au udhalilishaji," alisema Samia.

"Serikali tunafanya jitihada za kupambana na hili la unyanyasaji, lakini mpaka pale jamii itakapoamua kuwa wazi katika masuala haya ndipo itakapoishia," alisema Samia.

"Wanawake ambao tunaingia kwenye nyumba ambazo tunakuta watoto ambao mama yao ametangulia mbele za haki, tuache unyanyasaji na udhalilishaji, tuanze na sisi, unaingia kwenye nyumba ambayo watoto mama ametangulia, unaanza kuwanyanyasa, kuwatumikisha makazi makubwa, huwapendi, ingekuwa wewe mwanamke mwenzio anafanya hivyo ungejisikiaje."

Samia aliongeza: "Tuwe na hofu ya Mungu, hakuna atakayekaa milele, mwenzio katangulia na wewe iko siku utakwenda, lakini utakwenda na zigo la dhuluma umebeba mgongoni utakwenda kumwambia nini Mungu. Niombe wanawake tusimamieni haki zetu, mtoto wa mwenzio ndio wako."

Miongoni mwa maazimio hayo ya Beijing ambayo alisema Tanzania imefanya vizuri ni pamoja na kupambana na suala la umaskini kwa wanawake, elimu na mafunzo kwa wanawake hao, na kwamba takwimu zinaonyesha imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuupunguza.

"Ile tu kusema Tanzania inatoa elimu bila malipo ni ukombozi mkubwa sana kwa watoto wa kike kwa sababu kabla ya hapo waliokuwa wanakwenda zaidi shule ni watoto wa kiume na waliokuwa wakiumia ni watoto wa kike," alisema Samia.

Mambo mengine ni katika sekta ya afya ikiwamo huduma ya mama na mtoto, haki za wanawake, nyanja ya kisiasa na kwamba katika suala la maamuzi Tanzania inaendelea kulifanyia kazi kuhakikisha kundi hilo linashiriki zaidi katika eneo hilo.

## Sababu mfumuko wa bei kushuka

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MFUMUKO wa bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia Februari 2021 umepungua kutoka asilimia 3.5 kwa mwaka ulioishia Januari, 2021 hadi kufikia asilimia 3.3 kwa mwaka ulioishia Februari, 2021.

Hayo yalibainishwa jana Dodoma na Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii, Ruth Minja, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mfumuko wa bei.

Alisema, kushuka kwa mfumuko wa bei kunamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia Februari 2021 umepungua ikilinganishwa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia Januari 2021.

Alifafanua zaidi kuwa kupungua kwa mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Februari 2021 umechangiwa hasa na kupungua kwa bei za baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula kwa kipindi kilichoishia Februari 2021 zikilinganishwa na bei za mwezi Februari 2020.

Alisema baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizopungua bei kwa mwezi Februari 2021 zikilinganishwa na bei za Februari 2020 ni samani, kwa asilimia 5.3, mafuta ya taa kwa asilimia 15.7, vifaa vya nyumbani kama pasi ya umeme kwa asilimia 4.7, vyombo vya ndani kwa asilimia 3.3, dizeli kwa asilimia 22.8,petroli kwa asilimia 13.4.

Hata hivyo, alisema mfumuko wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwezi Februari 2021 umeongezeka kutoka asilimia 2.8 mwezi Januari 2020 hadi asilimia 3.6.

**HABARI KITAIFA**

# TAKUKURI yataja vishawishi vya rushwa ya ngono vyuoni

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imebainisha mbinu zinazotumika kushawishi rushwa ya ngono katika vyuo vikuu kuwa ni kutoa alama za chini kwenye mitihani, vitisho vya kutofaulu kwa wanafunzi, kutoa ahadi kama kumpatia ajira, cheo na chumba chuoni.

Ushawishi mwingine ni nafasi ya uongozi, kuongezewa alama za ufaulu au kusaidia kupata ufadhili wa masomo, kuchelewesha utoaji wa huduma na wahadhiri kuwaita wanafunzi kwenye mazingira yasiyo rasmi kwa ajili ya kukagua kazi zao.



Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo (pichani), alibainisha hayo kupitia ripoti ya utafiti wa rushwa ya ngono vyuoni, waliofanya mwezi uliopita katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Dodoma (UDOM) na kuwasilisha kwa vyombo vya habari jana ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Mwanamke Duniani.

Alisema lengo kuu la utafiti huo ni kupata taarifa za kisayansi zitakazosaidia kukabiliana na kero ya rushwa ya ngono katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini.

"Tatizo la rushwa ya ngono kwenye vyuo lipo; wanafunzi asilimia 58 na watumishi asilimia 69 walieleza kuwapo kwa matukio ya vitendo vya rushwa ya ngono," alisema Brigedia Jenerali Mbungo.

Aidha, alitaja sababu za kukithiri kwa rushwa ya ngono vyuoni kuwa ni mifumo dhaifu ya kudhibiti matumizi mabaya ya mamlaka, mifumo dhaifu ya kusimamia uwajibikaji na mfumo dhaifu wa ajira hasa ajira za wahadhiri.

Sababu nyingine alisema ni ufinyu wa huduma muhimu kama hosteli; mikopo ya elimu kuongezeka kwa wanafunzi pamoja na mmomonyoko wa maadili kwa ujumla.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 7 (a) na (c) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba Il ya Mwaka 2007, TAKUKURU inao wajibu wa kufanya uchambuzi na kupitia taratibu za mamlaka ya umma na binafsi kwa nia ya kuiwezesha kubaini mianya ya vitendo vya rushwa, kushauri namna bora ya kuziba mianya iliyobainika kushirikiana na wadau kupambana na rushwa," alisema.

Alifafanua kuwa, baada ya kufanya utafiti huo waliitisha kikao kazi cha wadau cha kujadili matokeo ya utafiti na kuweka mikakati ya kuidhibiti kero hiyo.


## [redacted] NOTISI/ TANGAZO

WAUNGWANA AUCTION MART,NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTOR LTD, TAUSI AUCTION MART CHAMPION AUCTION MART LTD, SUNDI AUCTION MART LTD, SMARKCORE GROUP LTD , BEST GROUP LTD , SALEI AUCTION MART LTD kwa mamlaka tuliyo pewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tuna toa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| S/No | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SINDE TRAINING COLLEGE LTD | SINDE LIMITED | ENEO LA CHUO NA MAJENGO YAKE. | ILEMI,MBEYA JIJI | 23/03/2021 |
| 2. | JUHUDI JACKOBU MWAKISOLE | JUHUDI JACOBU | PAGALE LA NYUMBA | NSALAGA,MBEYA JIJI | 23/03/2021 |
| 3. | JOSEPH LAURENT SOJO | JOSEPH LAURENT SOJO | NYUMBA YENYE HATI ZA KIMILA | KATUMBA,RUNGWE, MBEYA | 24/03/2021 |
| 4. | **EMANUEL MHOPAJE MWASHIOZYA** | **EMANUEL MHOPAJE MWASHIOZYA** | NYUMBA | IYULA MBOZI ,SONGWE | 26/03/2021 |
| 5. | **HURUMA WAILES MBEMBELA** | **HURUMA WAILES MBEMBELA** | NYUMBA | IYULA MBOZI,SONGWE | 26/03/2021 |
| 6. | **FELIX MAVIKE MSIGWA** | **FELIX MAVIKE MSIGWA** | NYUMBA | ILEMI,MBEYA JIJI | 24/03/2021 |
| 7. | **CHARLES JOHN ZIMBA** | **CHARLES JOHN ZIMBA** | NYUMBA | NYIGAMBA,UYOLE, MBEYA JIJI | 25/03/2021 |
| 8. | **MASHAKA SINARAHA SHILELEMA** | **MASHAKA SINARAHA SHILELEMA** | KIWANJA CHENYE HATI | FOREST MLOWO,MBOZI SONGWE | 29/03/2021 |
| 9. | **ZANA NELSON MWALEMBE** | **ZANA NELSON MWALEMBE** | KIWANJA CHENYE HATI | FOREST MLOWO,MBOZI SONGWE | 29/03/2021 |
| 10. | **MARY ASAJILE MWAMWEZI** | **MARY ASAJILE MWAMWEZI** | NYUMBA | MLOWO MBOZI,SONGWE | 29/03/2021 |
| 11. | **WILLA JACOBU ZUNDA** | **NASSON MWAKALIMBILE SOTE** | NYUMBA | NZOVWE ,MBEYA JIJI | 27/03/2021 |
| 12. | REHEMA ALOYCE NDELWA | EPHRAIM GOVELLA | NYUMBA | HALI YA HEWA ,MBEYA JIJI | 27/03/2021 |
| 13. | YESAYA SAMWELI KIBONDE | YESAYA SAMWELI KIBONDE | NYUMBA | SHEWA,MBEYA MJINI | 03/4/2021 |
| 14. | OBONYO LAWRENCE SEDA | OBONYO LAWRENCE SEDA | NYUMBA | CHATEMBO,MWANDEGE – DAR ES SALAAM | 13/03/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0713077474
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.


# Mama Mwinyi ataka kupinga udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi, ameitaka Jumuiya ya Rafiki wa Wanawake na Watoto Zanzibar (RAWWAZA), kupitia kampeni yake ya 'Amka Mwanangu' kuendelea kushirikiana na serikali katika mapambano dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa watoto na unyanyasaji wa kijinsia.

Mama Mwinyi aliyasema hayo wakati akiizindua rasmi Kampeni ya 'Amka Mwanangu' iliyoanzishwa na Jumuiya ya RAWWAZA, hafla iliyofanyika, Malindi, jijini hapa.

Katika hotuba yake, Mama Mwinyi aliitaka jumuiya hiyo, kuwapa elimu watoto kuhusu njia bora ya kujikinga na vitendo hivyo na kuwafundisha taratibu za kisheria zinazopaswa kufuatwa kutoa taarifa za matukio ya udhalilishaji na upatikanaji wa ushahidi.

Alisema juhudi za jumuiya hiyo zina mchango mkubwa katika utekelezaji wa malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuimarisha haki, usawa pamoja na kuongeza fursa za kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa wanawake wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Aliwasihi wazazi kuwalinda watoto na kuzungumza nao vizuri na kuacha kutopokea zawadi ama rushwa baada ya mtoto kuathirika kwa kuwa vitendo hivyo vinawaharibu watoto kisaikolojia.

Alisema kutokana na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Nane, anaimani kwamba vitendo hivyo vitakuwa historia huku akisisitiza ushirikiano.

Aliwataka kuongeza nguvu ili kutekeleza kwa ufanisi dira na dhamira ya jumuiya yao pamoja na malengo ya Kampeni ya 'Amka Mwanangu' katika kipindi chote cha mwaka mmoja kuongeza ari na hamasa katika kuimarisha na kutetea maslahi ya wanawake na watoto pamoja na kuwa wabunifu kwa kuibua miradi yenye tija ili hatimaye isaidie kuongeza kipato cha wananchi.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Tauhida Cassian Gallos, alitaja mafanikio yaliyopatikana katika jumuiya hiyo ambayo yanatokana na malezi mazuri kutoka kwa walezi wa jumuiya hiyo ,pamoja na mapenzi na ushirikiano wa wajumbe wote wa jumuiya.


**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**INVITATION TO BID: NO. ITB 2021 001**

**FOR THE ESTABLISHMENT OF A FRAME AGREEMENT FOR THE PROVISION OF AUCTIONEERING SERVICES**

1. **Background:**
The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR invites reputable and qualified suppliers to submit firm offers for establishment of a frame agreement for provision of auctioneering services in Uganda, Tanzania, Chad, Cameroon, and Pakistan.

2. **Eligibility:**
Suppliers duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's requirements are invited to participate in the bidding process.

Kindly download the tender documents in the below link:

**UNGM:**
**https://www.ungm.org/Public/Notice/122493**

**UNHCR:**

**Cover:**
**https://www.unhcr.org/admin/sts/602e6bd04/invitation-bid-no2021itb001-establishment-frame-agreement-provision-auctioneering.html**

**Annexes:**
**https://www.unhcr.org/cgi-bin/texis/vtx/home/opendocAttachment.zip?COMID=602e6b894**

**CRUCIAL DATES FOR THIS INVITATION TO BID**

| | |
|---|---|
| **Deadline for receiving requests for clarification** | **Wednesday 03rd March 2021 at 23.59 hrs, CET** |
| **Deadline for submission of offers** | **Wednesday 17th March 2021 at 23.59 hrs, CET** |

UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.

HABARI KITAIFA

# Shule zafungiwa kulaza wanafunzi kisa mabweni

**Na Lilian Lugakingira**, KYERWA

SHULE mbili za msingi ambazo ni Kido na Talent wilayani Kyerwa mkoani Kagera, zimefungiwa kutoa huduma ya bweni, kutokana na majengo yake kutofaa kulaza wanafunzi.

Hatua hiyo imetokana na ukaguzi uliofanywa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa lengo la kujiridhisha kama wahusika wanazingatia kinga ya ajali za moto katika shule.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo uliozihusisha wilaya zote saba za mkoa huo kuanzia Februari 05 hadi 23 mwaka huu, Kaimu kamanda wa jeshi hilo Mkoa wa Kagera, Mkaguzi Thomas Majuto, alisema baadhi ya shule walikuta zina upungufu kidogo unaoweza kurekebishwa na kuepusha madhara.

"Lakini kuna shule ambazo tumekuta miundombinu yake imeharibika, haifai kulaza watoto, na kuna shule zimekutwa usajili wake ni wa kutwa, lakini zinalaza wanafunzi kimya kimya, tena katika mazingira ambayo hayana usalama," alisema.

Alisema shule ya awali na msingi ya Kido ilikuwa na mabweni ya kulaza wanafunzi 110, ambayo miundombinu yake ikiwamo kuta, madirisha, vitanda na milango vimechakaa na kupasuka.

"Lakini tumekataza deka tatu (kitanda kimoja kilichotengwa sehemu tatu za kulala yaani chini, katikati na juu), hii kwa mtoto mdogo wa darasa la pili au la tatu, linapotokea tatizo wakati wa kujiokoa anaweza kudondoka chini akakanyagwa au inaweza ikawa ngumu kuruka," alisema.

Kuhusu shule ya Talent, alisema ilisajiliwa kutoa elimu ya kutwa, lakini imekutwa ikilaza watoto katika mazingira yasiyofaa kutokana na jengo linalotumika kama bweni kuwa katika hali mbaya, na endapo ikitokea ajali, watoto wanaweza kuathirika.

"Katika shule zote mbili hazina vifaa vya kung'amua moto na kuzimia moto, wakati tumekuwa tukitoa elimu na maelekezo ili kunusuru maisha ya watoto, inaonekana baadhi ya shule hawazingatii," alisema.

Alitoa rai kwa mamlaka za elimu zinazohusika na ukaguzi wa shule kufanya kazi kwa juhudi na kwa umakini, maana suala la shule kuwa na kibali cha kutwa halafu ikalaza wanafunzi, ina maana kuna kujisahau, na kuwa ni vema wakapita na kufanya ukaguzi mara kwa mara.

"Lakini niwaombe wazazi, wanapokwenda kuandikisha watoto wao, wanapaswa kukagua mazingira ya shule kuona kama yanafaa kwa watoto wao, ili kujiridhisha kwa ajili ya usalama wa watoto," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa, Rashid Mwaimu, aliwataka wamiliki na wasimamizi wa shule zilizobainika kuwa na upungufu kufanya marekebisho haraka katika muda waliopewa, ili kuepuka adhabu.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akizungumza na wakazi wa Kata ya Kivule jijini Dar es Salaam jana, wanaolalamikia kucheleweshewa urasimishaji makazi yao na Chuo cha Ardhi Morogoro kwa muda wa miaka mitatu huku wakiwa wameshalipia pesa tayari. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Agizo kurejeshwa faru waliotoweka

**Na Lusungu Helela**, MOROGORO

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, ameiagiza menejimenti ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi kuhakikisha inawarejesha faru ambao walitoweka miaka ya 80, kutokana na kukithiri kwa vitendo vya ujangili.

Akizungumza jana mkoani Morogoro na menejimenti ya hifadhi hiyo, Dk. Ndumbaro alisema kwa kuwa faru hao walikuwapo kipindi cha nyuma, lakini tatizo la ujangili lilisababisha faru hao kutoweka kabisa.

Alisema hifadhi hiyo kwa sasa ina wanyamapori wakubwa 4 na sio 5 ambao ni simba, tembo, nyati na chui. "Kwanini faru hawapo katika hifadhi hii, je, mazingira sio rafiki kwao?" Alihoji Ndumbaro.

"Katika uongozi wangu, lazima nihakikishe Hifadhi ya Taifa ya Mikumi inakuwa "Big Five na sio Big Four", Menejimenti nataka kuwaona faru katika hifadhi hii kwani naamini wanaweza kuishi," alisisitiza Dk. Ndumbaro.

Alisema ikolojia ya hifadhi hiyo inaruhusu faru kuishi ikizingatiwa kipindi cha nyuma waliishi, hivyo kurejeshwa kwao kutasaidia Hifadhi ya Mikumi kuwa hifadhi bora zaidi kwa vile itakuwa imesheheni kiu ya watalii wenye matamanio ya kuona wanyamapori wakubwa wote katika hifadhi hiyo.

Ameagiza kuwa baada ya faru hao kurejeshwa katika hifadhi hiyo, ni lazima ulinzi uimarishwe maradufu ili kosa lililotokea kipindi cha nyuma lisijirudie.

Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania( TAWIRI), Dk. Gabriel Ottawa, alisema inawezekana faru watakaorejeshwa wataweza kuishi vizuri kwa vile kipindi cha nyuma faru hao walikuwapo katika hifadhi hiyo.

Aliahidi mbele ya Waziri kuwa watafanya kila liwezekanalo kwa kufanya utafiti mbalimbali kabla ya kuwaleta faru hao ili kujua changamoto pamoja na kuzitafuta ufumbuzi.

# Leseni za makazi ndani ya siku 14

**Na Hassan Mabuye**, MWANZA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeanza kutekeleza mradi wa utambuzi wa kila kipande cha ardhi kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi kwa kutoa leseni za makazi ndani ya siku 14.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo wa utambuzi na utoaji wa leseni za makazi katika viwanja vya Shule ya Msingi Mabatini Wilaya ya Nyamagana, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Angeline Mabula, alisema kuwa serikali imekusudia kuwatambua wananchi wote wanaoishi katika makazi ambayo hayajapangwa, hivyo kuwapimia na kuwamilikisha ardhi yao.

Alisema lengo la mradi huu ni kuondokana na changamoto za kukosa miliki ya ardhi kisheria, ikiwamo kuendeleza maeneo yao, huku akiwasisitiza wananchi hao kuhakikisha wanalipa kodi ya pango la ardhi baada ya kukabidhiwa leseni za makazi.

Aidha, Mabula aliwataka wananchi hao kuhakikisha wanaendeleza miliki zao kwa kufuata sheria na taratibu za mipango miji pamoja na kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati.

"Usipolipa kodi ya ardhi utaletewa ilani ulipe na ukiendelea kukaidi utapelekwa katika baraza la ardhi ulipe, ikifika miezi sita hujalipa sheria inamtaka ofisa ardhi mteule afute miliki yako bila hata kukwambia," alisema.

Kwa upande wake Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mwanza, Eliah Kamihanda, alifafanua kuwa mradi huu ujulikanao kwa jina la 'fit for purpose' una lengo la kutambua vipande vya ardhi vilivyoendelezwa bila kufuata sheria na taratibu za mipango miji (makazi holela).

Kamihanda aliongeza kuwa vipande vya ardhi 5,957 vinatarajia kutambuliwa na kumilikishwa kupitia utoaji wa leseni za makazi kwa mkoa wa Mwanza pekee, wakianzia Kata ya Mabatini, na kwamba tangu kuanza kwake Januari mwaka huu kwa kata hiyo vipande vya ardhi 111 vimeshatambuliwa na kutolewa leseni za makazi kwa wamiliki wake.

Naye mratibu wa mpango huo kutoka wizarani, Godfrey Machabe, aliongeza kuwa mpango wa kupanga, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi kwa kutoa leseni za makazi kwa kuanzia unatekelezwa katika mikoa miwili nchi nzima ikiwamo Mwanza na Arusha, hivyo kuwataka wananchi kutumia vizuri fursa hiyo ili kupata umiliki wa kisheria kwa vipande vya ardhi wanavyovimiliki.

## HABARI KITAIFA

# ACT yataka majadiliano soko Tanzania, Kenya

**Na Christina Mwakangale**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ametoa wito kwa serikali ya Tanzania na Kenya, kukaa meza moja kujadili soko la mahindi.

Amesema hatua hiyo italinda soko na uamuzi utakaotolewa dhidi ya Kenya baada ya kukataa mahindi nchini mwao, madhara ni makubwa.

Aliyasema hayo katika taarifa yake iliyotolewa na Idara ya Habari na Uenezi ya chama hicho jana, akibainisha kuwa Kenya na Tanzania ni ndugu na wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na kwamba mgogoro wowote unapaswa kutatuliwa kwa kutumia itifaki ya Soko la Pamoja la EAC.

"Mwaka 2017 Serikali ya Tanzania ilizuia mahindi kuuzwa nje. Maumivu waliyopata wakulima hayamithiliki. Kilo ya mahindi ilishuka mpaka Sh. 100. Nilipotembelea Wilaya ya Namtumbo nilikuta wananchi wanafanya 'barter trade' ya mahindi na mazao mengine kwa sababu mahindi hayakuwa na soko.

Wakulima wengi walitumbukia kwenye umaskini wa kutisha, wafanyabiashara walifilisika na msimu uliofuata mavuno yalishuka sana. Sitaki kuona mkulima wa Tanzania akirudi kwenye maumivu yale kwa serikali kushindwa kutimiza wajibu wake," alisema Zitto.

Pia alisema uamuzi wa kuzuia mauzo ya mahindi nje ya nchi, ulikuwa na makosa na kwamba Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, itimize wajibu wa kuzungumza na Wizara ya Mambo ya Nje ya Kenya, kwa kuzingatia Mkataba wa Afrika Mashariki.

"Sisi kama viongozi wa kisiasa wajibu wetu ni kwa Watanzania. Wajibu wetu sio kwa wengine zaidi ya raia wetu. Mahindi ya Tanzania ni salama, Watanzania hawalimi mahindi yenye sumu.

Watanzania wanakula mahindi haya haya yanayouzwa Kenya ni lazima kuwalinda wakulima wa Tanzania na ni muhimu kulinda soko la bidhaa za Tanzania.

## Mabweni kuwatumbua maofisa elimu

**Na Happy Severine,** ITILIMA

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amewataka maofisa elimu wa sekondari na wakuu wa shule kukamilisha ujenzi wa mabweni mkoani Simiyu ifikapo Aprili 3, 2021, na wakishindwa watapoteza nafasi hizo.

Silinde alitoa maagizo hayo jana wakati wa ziara ya kutembelea baadhi ya shule katika wilaya za Itilima na Bariadi kukagua ujenzi huo na kushangaa kuona ujenzi haujakamilika, huku fedha zilizotolewa zikiwa zimeisha.

Alisema serikali ilitoa Sh. milioni 80 katika baadhi ya shule kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ili kuwasaidia wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu na hatarishi hasa wasichana. Aliongeza kuwa katika mikoa mingine ujenzi umekamilika kwa kiasi hicho cha fedha, lakini katika Mkoa wa Simiyu ameshangazwa kuona ujenzi ukiwa haujakamilika, lakini fedha zote zimeisha.

Naibu Waziri huyo alitembelea shule za sekondari Itilima wilayani Itilima, Nyasosi na Bariadi na kuwataka wakuu wa shule hizo na maofisa elimu wa halmashauri kuhakikisha wanakamilisha ujenzi kwa muda aliotoa, vinginevyo watavuliwa nyadhifa zao.

"Haiwezekani katika mikoa mingine wakamilishe kwa fedha hizo hizo, lakini Simiyu mmeshindwa, kwanza kama serikali hatutaleta fedha nyingine, tunataka ujenzi ukamilike na halmashauri ziwajibike kutafuta fedha za kukamilisha," alisema Silinde

"Hadi kufikia Aprili 31, 2021 ujenzi ukamilike na wanafunzi waanze kutumia, mkishindwa mkuu wa shule na ofisa elimu hamtakuwa na nafasi hizi tena, hatuwezi kuvumilia hali hii, kuna dalili kuwa fedha za serikali zimetumika vibaya," alisema Silinde.




Meneja wa Huduma za Masoko wa Tigo, William Mpinga, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa maadhimisho ya miaka 10 ya huduma ya Tigo Pesa hapa nchini. Kushoto ni Mkuu wa Huduma za Tigo Pesa, Angelica Pesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Washtakiwa kusafirisha dawa za kulevya

**Na Hellen Mwango**

WAJASIRIAMALI, Anadhati Mchongea (20) na Emmanuel Msakuzi, maarufu kama Makuzi (23), wamefikishwa mahakamani kujibu mashtaka ya kusafirisha dawa za kulevya aina na heroine gramu 239.25 na bangi gramu 112.09.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Kija Luzingana, alidai kuwa Januari 22, mwaka huu, eneo la Kauzeni, Kunduchi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam kwa pamoja walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya heroine gramu 239.25.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa siku na mahali pa tukio la kwanza, washtakiwa walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya bangi gramu 112.09.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi bado haujakamilika. Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Machi 22, mwaka huu na washtakiwa wapelekwe mahabusu.

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY
AT DAR ES SALAAM

BILL OF COST NO. 125 OF 2020

ACCESS BANK TANZANIA LTD ........................ DECREE HOLDER/APPLICANT
VERSUS
AUREKE COMPANY LTD.......................... JUDGEMENT DEBTOR/ RESPONDET

SUMMONS FOR PUBLICATION

TO:
AUREKE COMPANY LIMITED
THE JUDGEMENT DEBTOR.

**WHEREAS,** the above mentioned case has been fixed for mention **6th day of April, 2021 AT 09.00 AM** before **Hon. C. Kisongo –Deputy Registrar** you are required to appear in this court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that day aforementioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of Court this **26TH day of February, 2021.**

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY
AT DAR ES SALAAM

BILL OF COST NO. 126 OF 2020

ACCESS BANK TANZANIA LTD ........................ DECREE HOLDER/APPLICANT
VERSUS
OMBENI LUKA MFARIJI.......................... JUDGEMENT DEBTOR/ RESPONDET

SUMMONS FOR PUBLICATION

TO:
OMBENI LUKA MFARIJI
THE JUDGEMENT DEBTOR.

**WHEREAS,** the above mentioned case has been fixed for mention **6TH day of April, 2021 AT 09.00 AM** before **Hon. C. Kisongo –Deputy Registrar** you are required to appear in this court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that day aforementioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of Court this **26TH day of February, 2021.**

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mwanamke chachu ya maendeleo, aaminiwe ashike nafasi uongozi

**JANA** yalikuwa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani chini ya kauli mbiu ya "Wanawake katika uongozi, chachu ya kufikia dunia yenye usawa," ikiwa ni kuonyesha ni kwa namna gani wanawake wanatakiwa katika nafasi za uongozi, na mchango wao ulivyo muhimu.

Jitihada nyingi zimefanyika katika kuhakikisha mwanamke anashiriki katika maendeleo anaonyesha uwezo wake mkubwa katika nyanja zote za maendeleo na siyo kwa kupendelewa, bali kutokana na uwezo wake wa kitaaluma na uzoefu.

Tangu Uhuru, Tanzania imepata makamu wa rais mwanamke, ambaye ni kiwakilishi tosha cha kuonyesha uongozi uliotukuka na namna gani mwanamke akiaminiwa, atafanya mabadiliko makubwa na kuiinua jamii yake, pia mwaka huu taifa la Marekani nalo limechagua makamu wa rais mwanamke, ambao wanakuwa mfano wa kuigwa kwa wasichana duniani.

Wapo wanawake ambao wameonyesha uwezo mkubwa kwa kuongoza kampuni, mashirika, vikundi na majimbo, na kupitia uongozi wao mafanikio makubwa yanaonekana, na ambayo yatabaki kwenye historia na kurithishwa vizazi na vizazi. Kama kauli mbiu inayoeleza, uhusiano wa uongozi na mwanamke kama chachu ya kufikia dunia yenye usawa, basi ni muhimu kuongeza idadi ya wanawake kwenye ngazi za maamuzi, kwa kuwa mchango wao ni thabiti na madhubuti katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Wapo wanawake katika sekta mbalimbali wenye uwezo wa kitaaluma, ujasiri na uzoefu mkubwa, wameteuliwa na kuchaguliwa katika nafasi za uongozi ambako wamefanya vizuri kiasi cha kuua dhana kuwa wanawake hawawezi hadi wawezeshwe au kuna upendeleo.

Kilichokuwa kimekosekana ni kuwajengea uwezo na kuwaamini kwenye nafasi wanazopewa au kuwapa nafasi kutokana na sifa zao, na siyo kwa sababu ni wanawake, na sasa waliopata nafasi hizo wamedhihirisha kuwa wanawake ni jeshi lenye uwezo mkubwa wa kuongoza na kuleta mabadiliko makubwa katika jamii.

Licha ya mafanikio hayo, bado idadi ya wanawake katika nafasi za uteuzi siyo za usawa, kwenye siasa hasa katika majimbo, ndani ya vyama vya siasa, ofisi mbalimbali na vyombo vya habari, jambo ambalo linadhihirisha bado kuna kazi ya kufanya kwa wote waliofanikiwa kufikia nafasi za juu za uongozi. Ni muhimu katika kuleta usawa kuongeza idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi zitokane na sifa zao, na siyo kutokana na jinsia zao, ili mchango wao kwenye uongozi uonekane.


Ili jamii iendelee, unahitajika mchango wa mwanamke na mwanaume, hivyo ni muhimu kuwapo usawa katika nafasi za uongozi kuanzia ndani ya vyama vya siasa ambavyo vinaunda uongozi wa chama na baadaye mchakato wa kupitisha majina ya watakaogombea katika nafasi za dola yakiwamo majimbo.

Tunatambua katika jitihada zilizofanyika za kuongeza idadi ya wanawake katika uongozi kutokana na Katiba ya nchi kuruhusu uwapo wa viti maalum, ambavyo vimesaidia idadi kubwa ya wanawake kuingia katika chombo cha kutunga sheria.

Pia tunatambua jitihada zilizofanyika ikiwamo mabadiliko ya sheria kama ya ardhi, ambayo inaruhusu wanawake kumiliki ardhi na umiliki wa pamoja kati ya wanandoa, ili kuondoa usumbufu na manyanyaso dhidi ya wanawake na watoto pale inapotokea baba amefariki na manyanyaso kwa mwanaume mama anapofariki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Uwepo mkakati kuandaa ufaulu duni kuwa 'vipanga'

**SEKTA** binafsi imepewa nafasi kushirikiana na serikali kutoa elimu ili Watanzania wapate elimu ingawa kumekuwapo na kasoro kadhaa kwenye ushiriki wao.

Miongoni mwa yanayonung'unikiwa ni shule binafsi kuwaacha wanafunzi wenye uwezo mdogo darasani na kukimbilia vipanga wenye ufaulu wa juu. Ni kweli katika kutoa elimu, shule binafsi zina mbinu mbalimbali za kuwawezesha kupata wanafunzi wengi zaidi kutokana na ukweli kwamba shule ni huduma, lakini zama hizi ni biashara na uwekezaji mkubwa.

Kuchukua wanafunzi waliofaulu zaidi ni miongoni mwa mbinu hizo zinazolenga kupata wenye uwezo mkubwa kutoka shule mbalimbali za msingi. Watoto wenye ufaulu wa juu wanaziwesha kuwa vivutio kwa wazazi kutokana na matokeo yanayofurahisha.

Mbinu hiyo na nyingine nyingi, inazifanywa shule hizo kuwa miongoni mwa zile bora kitaifa, kwa kufanya vizuri katika matokeo ya mitihani ya kikanda na kitaifa na kuzifanya ziendelee kuchangamkiwa na kupendwa.

Kinachofanywa ni kizuri katika biashara, lakini ni kikwazo kwa wanafunzi wenye uwezo mdogo darasani, kutokana na ukweli kwamba wanapochukuliwa wale wenye ufaulu wa juu tu ili kuziongezea sifa shule zao sifa wanabaki wapi?

Kwa mtazamo wangu mbinu au utaratibu huo ni mzuri, lakini bahati mbaya unawatenga wenye uwezo mdogo. Sasa hao watasaidiwa na nani ili nao wawe vipanga darasani?

Nia ya kuwa na wanafunzi wenye uwezo mkubwa ili shule hizo zifanye vizuri katika mitihani ya taifa ili kuvutia wazazi wengi zaidi kusomesha watoto wao ni jambo jema, lakini wahusika wasiweke huduma pembeni. Wenye uwezo mdogo nao wanatakiwa kusaidiwa ili kiwango chao cha uelewa kipande, lakini wanapoachwa na kuchukuliwa wenye alama za juu, ni sawa na kuwatenga.

Shule zinapochukua wanafunzi wenye alama za juu kutoka shule za msingi kwenda kidato cha kwanza sifa zinakwenda kwa sekondari iliyowachukua lakini zile zilizowaandaa hazijulikani tena. Suala la kuchukua wanafunzi wenye alama za juu na kuwacha wenye uwezo mdogo si zuri muda wote, hivyo kama zinataka kupata sifa halisi, zichukue hata wenye uwezo mdogo 'ziwatengeneze'.

Inaelezwa kuwa shule binafsi zina walimu wengi wenye sifa na vifaa vya kutosha vya kufundishia, si vibaya zikaanzisha programu maalum ya kuchukua wanafunzi bila kujali ufaulu na 'kuwatengeneza' kuwa bora zaidi.

Shule kujiwekea wastani mkubwa wa ufaulu unaosababisha baadhi ya wanafunzi kukwama, unaweza kuwa na manufaa kwa wachache na kuacha wengi wanaohitaji kusaidiwa wakaishia njiani. Wataalamu wa elimu wanasema, kila mwanafunzi ana na uwezo wa kuelewa masomo, ila tatizo ni kutotambua kuwa wana uwezo huo, hivyo njia pekee ni kuwasaidia wajitambue.

Lakini shule zinapotaka waliofaulu vizuri pekee maana yake ni kwamba wale wenye tatizo la kutotambua kuwa wana uwezo darasani, wataendelea kubaki nyuma iwapo juhudi za kuwawezesha hazitachukuliwa.

Njia mojawapo ya kumaliza tatizo hili ni serikali kuchukua wanafunzi wa madaraja yote A, B na C bila kujali kuwa wengi waliopata madaraja hayo wametoka katika shule binafsi.

Shule binafsi zisiwatenge wanafunzi wenye wastani mdogo. Pia serikali inaweza kufanya baadhi ya mambo ikiwa ni pamoja na kununua vitabu kwa ajili ya wanafunzi ili kila mmoja awe navyo, kwa ajili ya masomo yote ili kuwaongezea uelewa wasichwe nyuma. Kwa mazingira kama hayo, idadi ya wanafunzi wenye alama za wastani wa D, inaweza kupungua na kuwa na wanafunzi wenye upeo mkubwa wanasiochujwa na shule zinazotaka wenye ufaulu wa juu.

Inawezekana baadhi ya wazazi wakahamisha watoto wao kwenda katika shule ambazo wanaamini kuwa zina ufaulu mzuri, lakini wenye wastani wa D nao wasiendelee kuachwa nyuma.

Wenye ufaulu wa chini wana haki ya kupata fursa ili wanapokwenda katika shule binafsi wachukuliwe, siyo kusubiri waliofaulu vizuri pekee huku wenye uelewa mdogo wakikosa sehemu ya kuandaliwa zaidi.

HABARI KITAIFA

## Tigo yaadhimisha miaka 10 mageuzi huduma fedha

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu ya Tigo Tanzania, imesherehekea miaka 10 ya Tigo Pesa, huduma kamili ya kifedha inayohudumia zaidi ya wateja 9 milioni tangu kuanzishwa kwake.

Tigo Pesa imepitia mageuzi makubwa toka kuwa huduma ya kutuma na kupokea pesa hadi kuwa huduma kamili ya kifedha ikitoa huduma mbalimbali ikiwamo mikopo, bima, pamoja na malipo ya ankara.

Pia, kupitia uhuishaji wa huduma Tigo Pesa imewezesha huduma za kutuma pesa mitandao mingine, benki, mataifa mbalimbali pamoja malipo ya Serikali (GePG) zote zikiwa za kwanza kutoka Tigo Pesa katika soko la Tanzania.

Akizungumza wakati wa hafla iliyofanyika katika makao makuu ya Tigo jijini Dar es Salaa jana, Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, alisema: “Imekuwa safari ya aina yake ya kuboresha maisha ya mamilioni ya watumiaji wa huduma hii Tanzania, huku tukichangia katika ajenda ya ujumuishwaji wa watu kiuchumi kupitia mfumo wa ikolojia wa Tigo Pesa.”

“Huduma ya Tigo Pesa imeweza kutengeneza fursa za ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa zaidi ya mawakala 120,000 Tanzania nzima, ambao wanapata kipato kupitia kuwawezesha wateja kufanya miamala mbalimbali ambapo wamepokea jumla ya Sh. bilioni 692 kama kamisheni mpaka sasa,” alisema Pesha.

Kwa mujibu wa Pesha, miaka kumi iliyopita, muamala wa Tigo Pesa ulimaanisha kutuma na kupokea pesa, lakini leo hii Tigo Pesa imekuwa sehemu muhimu ya maisha ya kila siku ikitoa huduma mblimbali zinazokidhi mahitaji ya kifedha ya wateja.

# Mtumishi TANESCO kizimbani kesi uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

OFISA wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Jacob Ntupwa (51), amefikishwa mahakamani akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi na kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 48.

Mshtakiwa huyo akiwa mtumishi wa shirika hilo pia anakabiliwa na kesi ya wizi na kughushi.

Alisomewa mashtaka yake jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kati ya Januari 2015 na Oktoba 2018 ndani ya Wilaya ya Ilala, Kinondoni na Temeke jijini Dar es Salaam na Kibaha, mkoani Pwani, mshtakiwa akiwa mwajiriwa na TANESCO aliiba Sh. 48,264,357.06 mali ya serikali.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa mahali pa tukio la kwanza, mshtakiwa aliisababishia TANESCO hasara ya fedha hizo.

Wankyo alidai katika shtaka la tatu, mshtakiwa akiwa na nia ovu katika kipindi hicho cha kosa la kwanza, akiwa mtumishi wa shirika hilo, alibadilisha taarifa kwenye kompyuta na kutengeneza miamala (token) ya umeme na kujipatia faida kinyume cha sheria.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mashtaka yanayomkabili ni ya uhujumu uchumi.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuomba mahakama kupanga tarehe ya kutajwa.

Hakimu Shaidi alisema kwa sababu mshtakiwa anakabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumi, mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo mpaka kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP).

Alisema mshtakiwa apelekwe mahabusu mpaka Machi 3, mwaka huu kesi hiyo itakapotajwa.



Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo (katikati), akipanda mti kwenye eneo la Hifadhi ya Msitu wa Mazingira Asilia wa Kazimzumbwi, wilayani humo, mkoani Pwani jana, ikiwa ni sehemu ya tamasha la Kisarawe Ushoroba. Kulia ni Meneja wa Vodacom Tanzania Foundation, Sandra Oswald ambao ni wafadhili wa tamasha hilo na Mhifadhi Mazingira wa Mfuko wa Wanyamapori Duniani (WWF), Dk. Severin Kalonga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi waonywa ubaguzi watoto kufanyakazi

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, amewataka wazazi na walezi katika mkoa huo kuacha ubaguzi kwa watoto wao kuwachagulia kazi wa kike na kiume.

Alisema kufanya hivyo ni kuendelea kumbagua mtoto wa kike na kuendeleza mfumo dume kwenye jamii. Ndikilo aliyasema hayo jana katika Kijiji cha Kimanzichana, Wilaya ya Mkuranga kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Alisema wazazi wanatakiwa kuwahamasisha watoto wote bila kubagua jinsia zao kufanya kazi zote kwa bidii pia kuwahamasisha kusoma masomo yote ambayo yatakuwa msaada mkubwa kwenye maisha yao ya baadaye.

Alitoa onyo kwa wazazi na walezi wanaoficha watoto wa kike wenye ulemavu na kusababisha kuwanyima haki zao za msingi. Aliwasisitiza wananchi kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye jamii ikiwa ni pamoja na kukomesha vitendo vya mimba za utotoni.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2020 wanafunzi zaidi ya 130 wa mkoa huo wameshindwa kuendelea na masomo baada ya kupata mimba wakiwa shuleni, wanafunzi wa shule za msingi ni 39 na sekondari ni zaidi ya 100.

Ndikilo alisema kitendo cha wanafunzi hao kukatisha masomo ni kuendelea kumdidimiza mtoto wa kike.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Pwani, Grace Tete, alisema bado kuna matukio ya ukatili wa kijinsia ambayo yanaendelea kuripotiwa katika Ofisi za Ustawi wa Jamii.

Alisema takwimu zinaonyesha kwa kipindi cha mwaka 2020 wanawake 2,316 walifanyiwa vitendo vya ukatili kesi ambazo ziliwasilishwa kwa Ofisa Maendeleo ya Jamii na kuchukuliwa hatua.

Katika utekelezaji wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia wa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), mkoa umeendelea kufanya uhamasishaji wa uzalishaji wa kamati za ulinzi ngazi ya jamii.

Alisema lengo la mpango huo ni kuweka mazingira salama kwa wanawake na watoto katika maeneo yao na kuimarisha uchumi ambao umeonekana ni chanzo cha unyanyasaji kwa makundi hayo.

Alitaja vikwazo wanavyokumbana navyo kuwa ni pamoja na baadhi ya halmashauri kutochangia asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa wakati hali inayochangia ucheleweshaji wa utoaji wa mikopo kwa walengwa.

Vikwazo vingine alitaja kuwa ni pamoja na baadhi ya vikundi kutorejesha fedha za mikopo zinazotakiwa, uwapo wa kaya maskini ambazo hazijafikiwa na mpango kutokana na upungufu wa rasilimali fedha.

Katika maadhimisho hayo Mkuu wa Mkoa alikabidhi hundi zenye thamani ya jumla ya Sh. milioni 228 kwa vikundi vya wajasiriamali.

# Walia kupungua kwa samaki Ziwa Victoria

**Na Richard Makore,** MWANZA

CHAMA cha Wavuvi Tanzania (TAFU), kimeiomba serikali kufanya utafiti kubaini chanzo cha kupungua samaki katika Ziwa Victoria pamoja na kutatua mgogoro kati ya wavuvi wa dagaa na sangara.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa chama hicho, Bakari Kadabi, alipozungumza na Nipashe kuhusu maendeleo ya sekta ya uvuvi katika Ziwa Victoria.

Alisema samaki wamepungua katika Ziwa Vitoria, lakini hawajui chanzo chake, hivyo serikali kupitia wataalamu wake wafanye utafiti kujua tatizo.

Kadabi alisema mialo mingi wavuvi wanalalamika kwamba wakienda ziwani hawapati samaki kama siku za nyuma.

"Samaki ziwani hakuna, serikali ifanye utafiti wa kina kubaini chanzo chake ili kuwasaidia wananchi ambao anategemea kazi hiyo ili kuendesha maisha yao," alisema.

Kuhusu mgogoro kati ya wavuvi wa dagaa na sangara, aliomba serikali kuchukua hatua ili kuleta utulivu.

Alifafanua kwamba, wavuvi wa sangara wanalalamika kwamba njia wanazotumia wavuvi wa dagaa kuvua kwa kutumia mwanga wa taa za sola unakimbiza samaki.

Kutokana suala hilo wavuvi wamekuwa maadui wanapokuwa ziwani wakifanya shughuli zao za uvuvi.

Alisema serikali iangalie suala hilo kwa kuwa nchini Uganda uvuvi wa kutumia taa za sola umepigwa marufuku.

Alitaka watu wanaokamatwa wakifanya uvuvi haramu nyavu zao zitaifishwe badala ya kuwapiga faini na kuwaachia nyavu zao.



Mkurugenzi Mtendaji wa TBL PLC, Philip Redman (kulia), akiwa katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyoandaliwa na UN Global Compact Network Tanzania kwa kushirikiana na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wafundwa ubora wa biashara

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE wajasiriamali na wafanyabiashara wameshauriwa kuongeza jitihada zao zaidi katika kuboresha zaidi mawazo ya biashara sambamba na kuongeza ubora wa bidhaa zao, ili kuongeza ushawishi kwa taasisi za kifedha ziwakopeshe kwa urahisi.

Akizungumza wakati wa kufunga Maonyesho ya Wafanyabiashara wanawake Tanzania jijini Dar es Salaam kwa siku nne, Meneja Uhusiano wa Benki ya NBC, Consolatha Shayo, alisema taasisi za kifedha zinashawishika zaidi kutoa mikopo kwa kuzingatia ubora wa wazo la biashara na sio jina au jinsia ya mkopaji.

Alisema hiyo ndio sababu benki hiyo imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha inaendelea kuwaongezea ujuzi wajasiriamali hao ili kuboresha mawazo na bidhaa zao lengo kuwajengea uwezo utakaowezesha kufanya biashara zao kwa weledi na kutengeneza faida itayowawezesha kurejesha mikopo yao.

"Ndio maana kupitia wataalamu ambao tunawatumia kutoa elimu kwa wajasiriamali kupitia maonyesho kama haya, tumekuwa tukifundisha na kusisitiza sana juu ya umuhimu wa kujenga zaidi majina ya bidhaa zao kuliko majina yao binafsi, kwa kuwa taasisi za kifedha zinatazama zaidi biashara zao na sio jinsia wala majina yao binafsi," alisema Shayo.

Pamoja na kudhamini maonyesho hayo, benki hiyo pia iliandaa programu kadhaa za mafunzo kwa wajasiriamali ikiwamo kliniki ya biashara kwa kushirikisha taasisi na mamlaka mbalimbali ikiwamo Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Mkurugenzi wa Taasisi ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TABWA), Noreen Mawala, ambaye taasisi yake ndio iliratibu maonyesho hayo pamoja na kuipongeza benki ya NBC na wadau wengine kwa kuyafanikisha, alisema taasisi hiyo inaandaa safari ya mafunzo na maonyesho ya biashara katika nchi za Oman na Comoro ili kutoa fursa kwa wafanyabiashara hao kutangaza biashara zao katika mataifa hayo.

## Maelezo ya awali kesi ya Mwijaku Machi 24

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imeambiwa kwamba upelelezi wa kesi inayomkabili msanii wa maigizo, Bulton Mwemba maarufu Mwijaku, dhidi ya tuhuma za kusambaza picha za ngono mtandaoni, umekamilika.

Kadhalika, mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu, imepanga kuanza kusikiliza maelezo ya awali Machi 24, mwaka huu.

Awali upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Kija Luzingana, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika, na iliomba tarehe ya kutajwa.

Hakimu alisema kesi hiyo itasikilizwa maelezo ya awali Machi 24, mwaka huu na dhamana ya mshtakiwa inaendelea.

Katika kesi ya msingi, Mwijaku anadaiwa kutenda kosa hilo katika tarehe tofauti kati ya Septemba 17 hadi Oktoba 10, mwaka 2019, jijini Da r es Salaam.

Ilidaiwa kuwa katika tarehe hizo, alisambaza picha za utupu akitumia kompyuta yake kupitia mtandao wa WhatsApp.

## Ikungi yakamilisha madawati sekondari

**Na Mwandishi Wetu**

HALMASHAURI ya Ikungi, mkoani Singida imekamilisha utengenezaji na ukarabati wa madawati ya wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 57.4.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Justice Kijazi, mafanikio hayo ni kutokana na ushirikiano baina ya serikali, jamii na wadau wa maendeleo.

"Shule kwa kushirikiana na jamii wameweza kutengeneza seti mpya za viti na meza 883 zilizogharimu Sh. 57,395,000, hadi kufikia Machi 3, mwaka huu, vilivyotengenezwa ngazi ya shule na halmashauri ni 2,913, hivyo upungufu wa kidato cha kwanza hautakuwapo," alifafanua.

Kwa upande wa vyumba vya madarasa, Kijazi alisema kwa kushirikiana na jamii na wadau wa maendeleo miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu itakapokamilika itagharimu zaidi ya Sh. milioni 228.5.

Alisema kwa ushirikiano huo wamerejesha vyumba 10 vya madarasa vilivyobadilishwa matumizi, kukarabati vyumba 29 vilivyokuwa havitumiki kwa zaidi ya Sh. 14,500,000. Pia alisema ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja Shule ya Sekondari Dadu uligharimu Sh. milioni 24 ikiwa ni kutokana na mapato ya ndani, mfuko wa jimbo na nguvu za wananchi.

# Waziri aonya watumishi kushiriki kwenye ujangili

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imewaonya watumishi wasio waaminifu wa Jeshi la Uhifadhi Wanyamapori na Misitu ambao wamekuwa wakishirikiana na majangili kwa lengo la kuhujumu maliasili kuacha mara moja. Imesema vinginevyo atakayebainika atavuliwa nyazifa hiyo na kushtakiwa kama raia wa kawaida katika kesi ya uhujumu uchumi.

Badala yake imewataka watumishi hao kuendelea kutekeleza majukumu yao ya kukomesha ujangili na kudhibiti uvamizi wa meneo ya wanyamapori na misitu kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

**Utafiti wao umeonyesha kuwa penye uhalifu kuna njama ya pamoja kati ya wavamizi na watendaji wa taasisi zilizo chini ya wizara.**

Onyo hilo lilitolewa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, alipokuwa akizungumza na viongozi wa uhifadhi wa Jeshi hilo kwenye mkutano na wadau wa utalii kujadili kuhusu kuongeza idadi ya watalii na mapato yatokanayo na shughuli za utalii.

Alisema utafiti wao umeonyesha kuwa penye uhalifu kuna njama ya pamoja kati ya wavamizi na watendaji wa taasisi zilizo chini ya wizara hiyo na wanaposigana kwenye masuala ya utoaji wa hongo, watendaji hao wanawakamata wavamizi ndipo wafugaji ama wakulima wanapotoa malalamiko dhidi ya utendaji wao usioridhisha.

"Habari ya kwanza ni kumwondoa vyeo vya kijeshi, habari ya pili ni kumvua unifom (sare) za kijeshi na habari ya tatu ni kumfukuza kazi ili aende mtaani tuone kama huko atapokea rushwa, na kwenye hili tutakuwa wakali sana," alionya Dk. Ndumbaro.

Alisema asilimia 95 ya maji yanayotumiwa kuzalisha umeme nchini vyanzo vyake vinatoka kwenye hifadhi, hivyo mtu atakayebainika kuvamia mifadhi na kufanya shughuli za uharibifu kwa kuendesha shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo na ufugaji huyo kosa lake ni uhujumu uchumi kwa mujibu wa sheria.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TABWA), Noreen Mawala (kushoto), akikabidhi zawadi kwa niaba ya wanawake wajasiriamali nchini kwenda kwa Meneja Uhusiano wa Benki ya NBC, Consolatha Shayo (kulia) na Meneja Bidhaa na Huduma za Kibenki kutoka Benki ya NBC, Jonathan Bitababaje (katikati), ikiwa ni ishara ya kutambua mchango wa benki hiyo katika kuwasaidia na kuwawezesha wanawake wajasiriamali. **MPIGAPICHA WETU**

# Awataka wakazi Pemba kufuga samaki

**Na Suleiman Omar,** PEMBA

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM) Mkoa Kusini Pemba, Munira Khatibu, amewashauri wananchi wa maeneo ya Nanguji Jimbo la Kiwani, kuanza kufuga samaki.

Aliwashauri kutafuta vifaranga vya aina mbalimbali vya samaki ikiwamo vifaranga vya sato na sangara ambao wana soko kubwa.

"Sato na sangara wana nafasi nzuri kibiashara na kipato chake ni kikubwa kwa wanaofuga kwa vile samaki hao wanakuwa wakubwa wanapofugwa kwa mazingira haya ya kwetu," alisema Nanguli.

Alisema yeye kama mjumbe wa kamati ya kilimo na mifugo, atahakikisha anashawishi ili wapate vifaranga hivyo ambavyo vinatolewa bure.

Akijibu changamoto zinazowakabili wafugaji wa kambare katika eneo hilo la Nanguji Kisiwani katika Wilaya Mkoani alisema yuko tayari kuwasaidia kupambana na changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwamo kuwajengea uzio uliozunguka bwawa lao na kudhibiti wizi.

Mmoja wa wanzilishi wa kikundi hicho cha ufugaji, Salim Khamis, alisema kikundi chao kimekuwa kikitumika kama cha mfano katika ukanda huo wa mashariki kwani kuna watu wengi ambao sasa huenda kujifunza kwao.

Pia mbunge huyo alitoa Sh. 500,000 kwa kikundi hicho ili kuwaunga mkono katika uchimbaji wa mabwawa.

Aliwaahidi kumlipia gharama zote za masomo kijana moja katika kikundi hicho ili akasome namna ya kufuga kitaalamu kwa kuzingatia ubora unaokubalika na kwamba atakuwa karibu nao ili kuhakikisha mafanikio wanayotarajia yanafikiwana.

## Taasisi yatenga bilioni 50/- kuwakopesha wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya huduma za kifedha ya Faidika, imetenga zaidi ya Sh. bilioni 50 kwa ajili ya kuwakopesha wafanyakazi wa serikali na taasisi zilizothibitishwa kwa mwaka 2021.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Baraka Munisi, alisema jana kuwa mikopo hiyo inatolewa ndani ya siku mbili endapo mkopaji atatimiza masharti yaliyowekwa.

Alisema masharti hayo yanajumuisha kuwa na kitambulisho cha kazi, stakabadhi moja ya mshahara wa mwezi uliotangulia, taarifa ya akaunti ya benki kuanzia miezi miwili na kuendelea na picha moja ya pasipoti.

Munisi alifafanua kuwa wameamua kutenga kiasi hicho kikubwa cha fedha kwa ajili ya kuboresha maisha ya Watanzania. Alisema kuwa mikopo hiyo hutolewa kuanza Sh. 200,000 hadi milioni 70 na urejeshaji wake unaanzia miezi sita hadi 84.

"Pamoja na changamoto za miundombinu kwenye taasisi nyingi za fedha, Faidika inaamini kuwa kila mtu anastahili kupata huduma ya kifedha ndiyo maana tumepanua wigo kupitia mifumo ya kisasa zaidi ya teknolojia ili kuwafikia Watanzania wote kwa lengo la kuboresha maisha yao," alisema.

## Msitu wakiingizia kijiji mamilioni

**Na Said Hamdani,** LINDI

SERIKALI ya Kijiji cha Nandenje, Kata ya Mandarawe, Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi, imekusanya Sh. 489,012,447.8 kutoka rasilimali misitu inayohifadhiwa na kutunzwa kwa zaidi ya miaka mitano.

Kutokana na makusanyo hayo, halmashauri hiyo imenufaika kwa kupata mgao wa asilimia 10 ya makusanyo yake.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Rashidi Bakari Daudi, ameyaeleza hayo katika mahojiano na Nipashe, na kubainisha kuwa makusanyo hayo ni ya kipindi cha miaka mitano iliyopita, kuanzia mwaka 2014/2015 hadi 2019/2020 kutoka Msitu wa Matete uliopo kijijini hapo wenye ukubwa wa hekta 5,025,ambao una aina mbalimbali za miti, huku akiitaja michache kuwa ni mninga, tondoo na msekese.

Alisema mapato hayo yamepatikana baada ya kuvuna na kuuza SBM 443.669 za miti.

# Waranda mbao waomba zabuni halmashauri

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

VIKUNDI vinavyofanya kazi ya kuchomelea na kuranda mbao katika eneo la viwanda vidogo lililotengwa na Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga kwa ajili ya wajasirimali, vimeomba kupatiwa zabuni zinazotolewa na halmashauri ili kuendelea kujiinua kiuchumi.

Eneo hilo lipo Kata ya Zongomela likiwa na ukubwa wa hekari 2,100, hekari 500 zikiwa limepimwa zaidi ya viwanja 621 na kuvigawa bure kwa wajasiriamali na hekari 1,600 kwa ajili ya wawekezaji wakubwa.

Mohamed Omari, Mwenyekiti wa Kikundi cha Mshikamano, aliyabainisha hayo juzi walipotembelewa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Patrobas Katambi.

Omari alisema wamekopeshwa na halmashauri hiyo Sh. milioni 50, na kuwa awamu ya kwanza halmashauri iliwakopesha Sh. milioni 10, awamu ya pili Sh. milioni 40, ambayo wanaendelea kufanya marejesho.

**Halmashauri inashindwa kuwapatia tenda inazozitoa hasa za utengenezaji wa madawati, madirisha na milango.**

Alisema halmashauri inashindwa kuwapatia tenda inazozitoa hasa za utengenezaji wa madawati, madirisha na milango.

Naye Heri Ramadhani alisema baadhi ya wajasiriamali waliopewa viwanja bure na halmashauri wametelekeza viwanja na kurudi mjini, hivyo kusababisha kuendelea kukosa wateja waliokuwa wanakwenda kwao moja kwa moja katika eneo hilo kununua mahitaji.

"Mwanzo tulikuwa katikati ya mji na tuliendesha shughuli zetu vyema na kwa kuwa palikuwa finyu, halmashauri ilitutafutia eneo lililopimwa na kutugawia viwanja bure na gharama yetu ilikuwa kutafuta hati pekee, ila cha kushangaa baadhi yetu tumeanza kurejea mjini," alisema Ramadhani.

Ofisa Maendeleo ya Jamii eneo la Viwanda Zongomela, Nausia Nawita, alisema eneo hilo lina vikundi vya wajasiriamali 14 na mpaka sasa vimeshakopeshwa Sh. milioni 221.

Alisema kikundi cha Mshikamano mara ya kwanza kilipewa Sh. milioni 10 na baada ya kufanya marejesho kwa wakati kilikopeshwa tena Sh. milioni 40, ambazo wanaendelea na marejesho, na kwamba kila kikundi kikimaliza kufanya marejesha kinakopeshwa zaidi.

Katambi aliipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kwa kutenga eneo na kuligawa bure kwa wajasirimali vijana kama moja ya hatua kutengeneza mazingira ya ufanyaji kazi.

Alimtaka Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba, kuhakikisha anawapatia zabuni vikundi vya ujasiriamali kulingana na ujuzi wao ili kuendelea kukuza mitaji yao.

## Wizara yaanza kutekeleza maelekezo ya JPM

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, amesema wizara imeanza kutekeleza agizo la Rais John Magufuli la kutafsiri sheria na kanuni katika sekta ya uvuvi ili wadau wote waelewe kwa ufasaha.

Gekul alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati akifunga kongamano la wadau wa sekta ya uvuvi nchini.

"Baadhi ya wavuvi nchini wana uelewa mdogo wa sheria na kanuni zinazosimamia sekta ya uvuvi kunakochangiwa na kuandikwa kwa lugha ya kigeni. Bahati nzuri katika wizara yetu tulishaanza michakato ya kuhakikisha sheria zetu zinatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, haina maana yoyote kama kanuni tu inayosimamia masuala ya uvuvi imeandikwa kwa lugha ya Kiingereza," alisema Gekul.

## Bil. 123/- kupeleka maji mamia ya vijiji

**Na Vincent Tiganya,** TABORA

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), unatarajia kutumia shilingi bilioni 123.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji kwenye vijiji 649 vya Mkoa wa Tabora.

Miradi hiyo inatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo ambapo wilaya zitakazonufaika ni Uyui, Sikonge, Kaliua, Igunga, Nzega na Urambo.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Tabora, Hatari Kapufi, alitoa taarifa hiyo jana wakati wa kikao cha wadau cha kujadiliana mikakati ya uboreshaji wa huduma za upatikanaji wa maji vijijini.

Kapufi alisema kwa Wilaya ya Uyui wanatarajia katika miaka mitano ijayo wanatarajia kutumia Sh. bilioni 16.7 ambazo zitawezesha kutoka vijiji 55 hadi kufikia 188 ambavyo vitakuwa na uhakika wa majisafi na salama ifikapo 2025.




Mtaalamu wa masuala kidigitali, Lilian Flavian (katikati), akipokea zawadi ya kinywaji cha konyagi yenye mwonekano wa nembo ya mwanamke, badala ya nembo iliyozoeleka ya mwanaume shupavu ikiwa ni ishara ya kutambua weledi, ujasiri na taaluma za wanawake walio na mchango chanya kwenye jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania Distilleries yamkumbuka mwanamke

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA jitihada za kutambua weledi, ujasiri na taaluma za wanawake walio na mchango chanya kwenye jamii, kampuni ya Tanzania Distilleries Limited kupitia kinywaji chake cha Konyagi imebadili mwonekano wa nembo ya kinywaji hicho ikiwa na picha ya mwanamke katika nembo yake iliyozoeleka kuwa na alama ya mwanaume shupavu aliyenyanyua mikono juu.

Chupa hizi maalum zina nembo yenye mwanamke aliyenyanyua mikono juu na ujumbe wa kuwatakia wa Tanzania heri ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo huadhimishwa kila tarehe 8 ya mwaka, mwezi wa 3.

Akizungumza na waandishi wa habari, Meneja wa bidhaa hiyo, Pamela Kikuli, alisema: "Konyagi ni kinywaji kinachotumiwa na watu wa jinsia zote, lakini kwa upekee, imeamua kuunga mkono wanawake wa nguvu wenye ujasiri, weledi na uwezo wa kufanya vitu vingi ambavyo vimekuwa vikionekana kufanyika zaidi na wanaume kuanzia ufundi wa magari hadi uendeshaji wa kampuni kubwa."

Pamela ameongeza kwamba Konyagi imekuwa ikifahamika kama kinywaji kinachopendwa zaidi na wanaume, lakini kinywaji kinachofurahiwa na jinsia zote, hivyo kumekuwa na umuhimu wa kipekee kutengeneza nembo maalum katika kipindi hiki cha kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani ili kutambua ujasiri wao, uwezo wao wa kusimama kama wao pamoja na utaalamu wanaotoa katika kuchangia kuendeleza jamii inayowazunguka.

"Zaidi pia tumeamua kutambua wanawake 100 wenye ujasiri, weledi na mchango kwenye jamii ya Kitanzania na kuwazawadia vitu mbalimbali ikiwamo chupa hiyo yenye nembo mpya," alisema Kikuli.

Miongoni mwa wanawake hao ni waliotambuliwa michango yao na kupewa zawadi ni Esther Mongezi (Mtangazaji wa TV na Redio Kipindi cha Michezo), Hellen Kazimoto (Mwandaaji wa Matamasha ya Muziki) na Angellah Karashani (Mshauri wa Habari na Burudani) ambao walipata fursa ya kuhudhuria kipindi cha Friday Night Live cha East Africa TV & Radio siku ya Ijumaa kuzungumzia harakati zao, utaalamu wao pamoja na mchango wao katika jamii ili kuwahamasisha wanawake wenzao wenye ndoto waweze kuzitimiza kwa ujasiri bila uoga.

Wengine ni Leah Mollel (Mwanzilishi wa Starshine TV), Mwanaidi Msuya (DJ Sweet Lady) - DJ na Rachel Pallangyo ambaye ni Refa wa Mpira wa Miguu katika Ligi Kuu ya Tanzania Bara (VPL). Wote walizungumzia tansia walizopo ambazo zimekuwa na historia ya kuwa na wanaume zaidi, lakini wao wameweza kuvunja fikra hiyo kwa kuwa vinara katika tasnia zao bila woga.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 9, 2021
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI







Ukurasa 12

UN yaitaka dunia ione mwisho wa enzi nishati gesi, makaa ya mawe

TEKNOLOJIA

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

## Jasiri mwenye ulemavu wa kuona anayemudu mzigo mzito maishani

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

# Kuchafuliwa na tuhuma za uzushi vyazamisha baharini jahazi 50/50





Waziri Saada Mkuya Salum. **PICHA MTANDAO**

LICHA ya kinamama kuimba, kuhamasisha na kuwabeba wagombea kwenye uchaguzi mkuu tena wakisajiliwa kama wapigakura wakuu katika uchaguzi mkuu au mdogo, lengo la kufikia asilimia 50 kwa 50 katika ngazi za maamuzi halijafikiwa.

Mathalani Zanzibar kwa sasa ni asilimia 38 ya wanawake waliomo katika Baraza la Wawakilishi, hivyo kuna kazi ya kusaka asilimia 12 zinazosalia. Ni kitu gani kinachowakwamisha wanawake kuwa wanasiasa?

Baadhi ya mambo yanatajwa kuwa ni pamoja na kuzushiwa kashfa za uongo, kuhusishwa na ngono, kukosa pesa lakini wanawake wabunge viti maalumu kuwa ving'ang'anizi.

**KUZUSHIWA MAMBO**

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wajumbe Wanawake wa Baraza la Wawakilishi (UWAWAZA), Sada Mkuya, anasema wanawake hukumbana na matatizo mengi wanapogombea nafasi za uongozi hasa katika siasa ikiwamo kashfa za kuzusha kwa lengo la kuwakatisha tamaa na wapo wanaodharauliwa kutokana na maumbile yao.

"Wapo wanawake wanapogombea nafasi za uongozi hupewa maneno ya kukatisha tamaa mfano mimi mwenyewe wakati naomba kura katika mchakato wa kura za maoni wakati nilipogombea Jimbo la Kikwajuni wapo waliokuwa wamenizulia kuwa nimefukuzwa Jimbo la Welezo ambapo awali nilikuwa mbunge wa jimbo hilo, nisingekuwa jasiri ningeshindwa kujieleza na kuomba kura," anasema Mkuya.

Mkuya ambaye ni Waziri Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, na aliwahi kuwa Waziri wa Fedha Serikali ya Muungano, anasema elimu inahitajika kwa jamii kuhusu nafasi za uongozi kwa wanawake ili kuwaunga mkono na kuwachagua.

**MADAI YA UZINZI**

Kuhusishwa na tuhuma za uhusiano na ngono ni changamoto inayokwamisha juhudi za 50/50 Mwakilishi wa Amani, Rukia Ramadhan Mapuri, anasema yeye ni miongoni mwa wanawake waliokumbana na maneno ya kashfa wakati alipogombea jimbo hilo na kueleza kuwa wengi wanaamini kuwa mwanamke anapoungwa mkono na mwanaume katika nafasi za uongozi anahusishwa naye kiuhusiano.

"Mimi ni mwathirika hasa wa hilo nilirushwa hadi katika mitandao ya kijamii kwa kashfa mbalimbali, lakini sikuvunjika moyo na nilipambana na hatimaye nikashinda katika uchaguzi mkuu," anasema.

**WASOMI WAWATISHIO**

Diwani wa Viti Maalum, Thuwaiba Jeni Pandu, anasema hofu dhidi ya wanawake wasomi ni miongoni mwa vikwazo vikuu vinavyowakabili wanawake kushika nafasi za uongozi Zanzibar.

Anasema kuibuka kwa wanawake wengi waliosoma na wenye uwezo katika maeneo mbalimbali imeleta hofu kubwa kwa baadhi ya wanasiasa wakongwe ambao wanajitahidi kuwafanyia kauzibe.

"Wanasiasa wakongwe wanahofu kubwa dhidi ya kuwapo kwa wanawake wasomi na ndio maana tumeshuhudia baadhi ya majimbo wanasiasa wakongwe ambao ni wanaume wameangushwa na wanawake na kushika nafasi majimboni," alisema.

**WANAWAKE VING'ANG'ANIZI**

Yumna Mmanga anayetoka Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar, anasema zipo changamoto nyingi zinazowakabili wanawake katika kugombea nafasi ya uongozi majimboni na hata katika viti maalum.

Yumna pia aligombea nafasi ya ubunge wa viti maalum vya watu wenye ulemavu kupitia CCM katika uchaguzi huo, anasema changamoto katika viti maalum zinatokana na wanawake wenyewe hawajawa tayari kuachia nafasi hizo ili sura mpya ziingie, badala yake wamebaki kuzitetea kila wakati.

"Hizi nafasi maalum ni kwa ajili ya kuwajenga wanawake ili kwenda kugombea majimboni, lakini wanawake wakishapata viti maalum huwa wanang'ang'ania hapohapo kipindi chote," anasema Yumna, mwenye ualbino.

**FEDHA NI SHIDA**

Ni changamoto kwa sababu kuna gharama ambazo zinahitajika katika mchakato wa uchaguzi kuanzia siku ya kwanza hadi kutangaza matokeo bila fedha hakuna kitakachofanyika, anaongeza Yumna. Anaongeza:

"Kutokana na ulemavu wangu sikuweza kutembea mchana kwenda kuomba kura kwa wajumbe wa viti maalum kutokana na jua kali na ilinilazimu nitembee usiku kuomba kura, lakini ilinibidi nitafute wa kuongozana naye na ilinibidi nimgharamie usafiri."

Aidha, anavitaka vyama vya siasa kubadili mfumo wa nafasi za viti maalum kwa kuweka muda maalum wa kushika nafasi hizo ili kutoa nafasi kwa watu wengine.

Wanawake wengi kipato chao ni kidogo tofauti na wanaume na ilimbidi azunguke mkoa mzima wa Mjini Magharibi kuomba kura na ilimbidi akodi gari kwa ajili ya usafiri na kwamba licha ya usafiri huo wa kuzunguka mkoa mzima, lakini kuna gharama ya kwenda Dodoma kwa ajili ya uchaguzi wa mchakato wa viti maalum lakini kwa wenye ulemavu inabidi kupata wasaidizi wengi na ni gharama zaidi.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Zakia Mohamed, anasema wakati umefika sasa kwa wanawake kujitoa zaidi katika kufikia maendeleo.

Anawataka wanawake waliopewa nafasi za uongozi kuzitumia vyema ikiwa ni pamoja na kujua shida za watendaji wa chini ili kufikia maendeleo ya taasisi.

"Uongozi ni dhima kubwa katika kufikia maendeleo ya dhati, ili kwenda sambamba na maendeleo hayo hakuna budi kuona kuwa wanatatua changamoto kwa wanaowaongoza," alisema.

**UCHUMI**

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa Ally, anasema uwepo wa takwimu sahihi za kiuchumi kwa wanawake utasaidia kukuza ustawi wa wanawake na kuweka mipango mizuri ya maendeleo visiwani Zanzibar. Anasema hadi sasa Zanzibar hakuna takwimu sahihi za kiuchumi ambazo zinaonyesha kipato cha mwanamke hali ambayo inapelekea kutojua uhalisia wa ongezeko la pato

INAENDELEA UK.12

TEKNOLOJIA

NA GAUDENSIA MNGUMI

# UN yaitaka dunia ione mwisho wa enzi nishati gesi, makaa ya mawe



Viwanda vya chuma vinavyotumia makaa ya mawe ni chanzo cha magonjwa ya njia za hewa na joto duniani linalochochea mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: MTANDAO**

MATUMIZI ya nishati ya visukuku (fossils) ambayo ni mabaki ya kale ya wanyama na mimea yanayofunikwa ardhini yanasababisha uchafuzi wa hewa na kuwa chanzo cha kifo cha mtu mmoja kati ya watano kila mwaka duniani kote.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio- Guterres, anasema na kuonya kuwa kuacha nishati za visukuku kama gesi asilia, makaa ya mawe na mafuta mazito na kuelekea kwenye nishati salama ni jibu la kuwa na afya njema na dunia isiyotishiwa na mabadiliko ya tabianchi.

Anaongeza kuwa kuachana na uzalishaji nishati kwa kutumia makaa ya mawe ni jawabu kwenye kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la joto duniani.

Magonjwa ya hewa yanayotokana na moshi wa visukuku, hasa makaa ya mawe yasiyochujwa kwenye upishi, uzalishaji wa nishati kama umeme, kupikia mafuta ya taa yanaweza kusababisha kuvimba na kupasuka kwa mifuko ya hewa kwenye mapafu na hivyo kupunguza uwezo wa mapafu wa kuingiza oksijeni na kutoa karboni au hewa ukaa kwa ufanisi.

Moshi huo pia husababisha kukusanyika makohozi kunakoambatana na kikohozi chenye uchungu na usumbufu na kupelekea matatizo ya kupumua. Wakati mwingine husababisha nimonia na dalili zote za changamoto za mfumo wa upumuaji, ikiwamo kukohoa, kukoroma na kohozi linalokaba koo na upumuaji wa viwango vya chini.

Katibu Mkuu wa UN, Antonio-Guterres, akihutubia kwa mtandao mkutano wa wadau wa makala ya mawe ulioandaliwa na Uingereza na Canada anasema utekelezaji wa mambo hayo matatu ni muhimu kwa kuwa tayari imebainika kuwa kuachana na matumizi ya nishati itokanayo na makaa ya mawe au visukuku, ni miongoni mwa njia za msingi zaidi za kudhibiti ongezeko la kiwango cha joto duniani ili lisizidi nyuzi 1.5 katika kipimo cha sentigrade.

Kuongeza hali ya joto duniani sasa kunaelekea kufikia nyuzi 1.5. Wataalamu wanaamini kuwa hali hiyo ikiachiwa itafikia nyuzi 2.0 na madhara yake ni makubwa na mojawapo ni mvua kubwa au haba zisizotabirika. Zinaweza kuambatana na mafuriko na vimbunga. Lakini joto linaweza kuwa kubwa, ukame wa muda mrefu, upepo na jua kali linaloambatana na ongezeko la maradhi na wadudu wanaoharibu mazao.

"Hii ina maana kuwa uzalishaji umeme kwa kutumia makaa ya mawe lazima uwe chini ya asilimia 80 ya viwango vya mwaka 2010 ifikapo mwaka 2030. Zamani za kale makaa ya mawe yalileta umeme kwa gharama nafuu kwa maeneo mengi na ilikuwa ni fursa ya ajira.

Siku hizo hoja hizo zimepitwa na wakati. Zaidi ya nusu ya uwezo wa kuzalisha nishati jadidifu au salama ulioongezwa mwaka 2019 ulifanikisha upatikanaji umeme kwa gharama nafuu kuliko mitambo mipya ya makaa ya mawe.

Nishati ya visukuku inachafua hewa na kuwa chanjo cha kifo cha mtu mmoja kati ya tano kila mwaka duniani kote.

Amekumbusha kuwa mkutano wa karibuni wa 'The 2021 United Nations Climate Change Conference au COP26, umeeleza kuwa dunia ina hali mbaya kwenye ulinzi wa mazingira unaochochewa na mabadiliko ya tabia nchi.

Mkutano wa 26 wa COP 26 unatarajiwa kufanyika Glasgow nchini Scotland, Novemba 2021 na hivi karibuni kuelekea COP26 imewekwa bayana kuwa mwelekeo wa kudhibiti ongezeko la joto duniani bado si mzuri kwa hiyo ni lazima kuchukua hatua za kijasiri ikiwamo kuachana na umeme wa visukuku.

**IAEA NA MBINU BUNIFU**

Katibu Mkuu amesema gharama ya kuunda mtambo wa nishati salama ni nafuu kwa kuwa hata Shirika la Umoja wa Mataifa la Nishati ya Atomiki (IAEA), limebaini gharama nafuu ya ujenzi wa mtambo mpya wa sola kwa unafuu badala ya kutumia mtambo wa makaa ya mawe.

"Nchini China na India, gharama za mtambo wa nishati salama inakuwa nafuu kila uchao. Hii leo natoa wito kwa serikali, kampuni binafsi na mamlaka za mitaa kuchukua hatua tatu," anasema Guterres.

Guterres anataka kusitishwa miradi ya makaa ya mawe na kueleza kuwa uwekezaji mpya wa makaa ya mawe ukome na watu waache uraibu wa matumizi ya makaa hayo.

Aidha, amewahimiza wanaogharamia kuachana na ufadhili wa makaa ya mawe na kwamba fedha za kuwekweza kwenye miradi ya makaa ya mawe zielekezwe kwenye miradi mipya ya nishati rejelezi au salama asikie, "nasihi za viongozi wa nchi zinazoongoza kwa kutoa hewa chafuzi wakitangaza kuachana na usaidizi wao wa kimataifa ya makaa ya mawe mapema mwaka huu na usaidizi zaidi uelekezwe kwa nchi zinazoendelea ambazo zinajitahidi kutumia nishati salama kufikishia huduma wananchi wao."

KIPINDI CHA MPITO

Katibu Mkuu wa UN anataka juhudi za pamoja za kuondokana na makaa ya mawe na kuelekea katika mitambo ya nishati salama zianze akisema kipindi cha mpito kitakachotoa fursa ya kutoka mtambo mmoja hadi mwingine akisema.

"Utafiti umeonyesha kuwa licha ya kwamba ajira zitapotea kwa kufungwa kwa mitambo, kipindi cha mpito kitawezesha kuzalishwa kwa mamilioni ya ajira ifikapo mwaka 2030."

Katibu Mkuu anasema Umoja wa Mataifa kwa upande wake utaunga mkono hatua za mpito na juhudi za kuhakikisha kuwa jamii zinazoingia kwenye marekebisho hayo zinachipuka na kustawi.

***HABARI ZA UN***

# Kuchafuliwa, tuhuma za uzushi vyazamisha baharini jahazi 50/50

**INATOKA UK.11**

kwa jamii hususani wanawake kwa kuwa takwimu hizo hujumlishwa kwa watu wote na hakuna mgawanyo wa jinsia. "Pamoja na mafanikio makubwa ya wanawake katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa, bado kuna changamoto zinazowakabili katika kufikia malengo yao," anaongeza Mzuri.

Anazitaja baadhi ya changamoto nyingine zinazowakabili wanawake ni dhana potofu ya jamii kudhani kuwa mwanamke hawezi kushika nafasi za uongozi akisema mitazamo hiyo imepelekea wanawake wengi wenye uwezo kukosa fursa muhimu ambazo zingewafanya kuwainua wanawake wenzao pindi wangepatiwa fursa hizo.

**ELIMU KISAIKOLOJIA**

Akizungumzia Elimu Mkurugenzi wa TAMWA, Rose Reuben, anasema elimu ya saikolojia kwa wanawake waliogombea nafasi za uongozi hasa katika siasa inahitajika kwa sababu wanakumbana na vitendo vingi ambavyo huwaathiri kisaikolojia.

Anasema wanawake waliogombea nafasi za uongozi katika siasa ikiwamo ubunge, uwakilishi na udiwani hukumbana na kashfa mbalimbali ili kukatishwa tamaa kutokana na kashfa za uongo kwa lengo la kukatishwa tamaa kutofikia malengo.

"Yapo baadhi ya maneno ya kashfa huwakumba wanawake wanaogombea nafasi za uongozi hivyo ni vyema kupatiwa elimu ya saikolojia hasa wanawake waliogombea," anashauri.

Aidha, anasema wanawake ni miongoni mwa waathirika wakuu wa unyanyasaji wa kijinsia hivyo aliwataka waliomo katika vyombo vya maamuzi kushirikiana katika kupeleka ajenda ya kuvunja ukimya dhidi ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake.

## SIKU YA WANAWAKE DUNIANI
## NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Jasiri mwenye ulemavu wa kuona anayemudu mzigo mzito maishani

- Mwalimu shule, mzazi pekee wa watoto
- Alfajiri safari mjini; nyumbani tuisheni



"NINATUMIA uzoefu na ninakariri sana, iwe sauti, milio, kila kitu ili kufika eneo fulani," ni maneno ya ufunguzi kutoka kinywani mwa mwanamama Regina Sylvester (pichani), jijini Dar es Salaam," anayeendelea na ufafanuzi:

"Mfano nikija nyumbani kwako, lazima nijue tangu nimeshuka kituoni na kufika ndani mwako pakoje mazingira kwa hisia, hata kwa kuhesabu hatua, palipo na ngazi natambua."

Ni kauli ya mkazi huyo wa Gongo la Mboto, nje kidogo mwa jiji hilo, mwenye ulemavu wa macho katika mazungumzo yake na Nipashe, mahususi anapoadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, inayofanyika kila tarehe kama ya jana ya mwaka.

Regina anaelezea masuala kadhaa yakiwamo ya maisha yake ya kila siku, ikiwamo kujitafutia riziki na kukabili changamoto zinazomtokea.

"Siku wa wanawake tuliitwa baadhi ya watu wenye ulemevu, tulihudhuria mkutano ulioandaliwa hapa jijini, pia ilikuwa ni fursa kuzungumza kuhusu changamoto za wasichana, wanawake na tulio na ulemavu.

"Kila mmoja alisema anachokiona, lakini mimi nilisema utakuta mtu haoni, anauza duka lake ila watu hawafiki dukani kununua vitu na kumuungisha, kutokana na dhana, imani potofu yaani mwenye ulemavu, wengine sijui wanatuchukuliaje," anaeleza.

Anaongeza: "Binadamu wote ni sawa, haki sawa, jamii, serikali ituangalie na sisi tuna haki."

**MAGUMU**

Pia, anataja changamoto wanazokumbana nazo mabinti wadogo, ikiwamo vishawishi vinavyosababisha kutofikia malengo yao.

Regina ambaye kitaaluma ni mwalimu, wa ngazi ya stashahada aliyopata kutoka Chuo cha Ualimu, jijini kilichopo jijini Dar es Salaam, analalamika amekosa ajira rasmi tangu ahitimu, kwake akiitafsiri kuwa changamoto ya pili kwake.

"Nimesomea St. Mary's kwa miaka mitatu tangu 2015, lakini sijawahi kupata ajira 'permanent' nafundisha tu twisheni mara chache nikiwa nyumbani, mwanafunzi mmoja Sh. 500 ananilipa kuliko kukaa tu, nimeweka kiasi kidogo," anasema.

Regina, anasema pia ana mtoto mmoja anayemlea peke yake pasipo usaidizi wa mzazi mwenzie, jambo linalomwacha katika magumu yampayo ujasiri wa kujitafutia kipato, ikiwamo kila siku alfajiri kwenda Kariakoo, iliko Shule ya Msingi Mchanganyiko, anakofundisha si kwa mkataba wa kudumu.

"Naamka saa 11 alfajiri, kufuata treni la abiria maarufu la 'Mwakyembe'. Natembea mwenyewe hadi kituoni. Ninatumia uzoefu kutambua maeneo, ninatakiwa kukariri sana kila ninapofika sehemu kwa mara ya kwanza eneo fulani.

"Hapo akili inatumika zaidi na si kingine na wala hatufundishwi shuleni, labda tulio na ulemavu namna ya kukariri maeneo zaidi. Tunafundishwa namna ya kutumia fimbo nyeupe (white canes) maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu, kabla ya kuvuka barabara au kubaini kuliko na miinuko, mabonde," anasema Regina.

Awali, Regina anasema alijikita katika ujasiriamali na kutengeneza sabuni za maji kwa ajili ya kufanya usafi na ingawa biashara haikuwa nzuri kama alivyotarajia.

"Nina mtoto ambaye anasoma 'baby class' (chekechea) kwa sasa. Ninamsomesha mwenyewe kutokana na kile ninachokipata na nimepanga, mume wangu niliyezaa naye tena tulifunga ndoa, tuliachana," anasimulia picha kuu ya maisha yake.

Anasema amekuwa akifundisha shule ya Uhuru Mchanganyiko iliyopo Kariakoo jijini kwa wanafunzi kuanzia darasa la tatu hadi saba, tangu Februari mwaka huu.

Ingawa Regina anasema kwamba malipo ni tatizo katika ajira hiyo, anandelea kufundisha pamoja na wenzake watatu, anaowataja wakazi wa Mbagala na Gongo la Mboto.

"Huwa najihimu alfajiri saa 11, napanda treni kwenda hadi Kariakoo, nashuka pale Gerezani natembea mwendo kidogo hadi shuleni.

> Nakutana na changamoto ikiwamo wakati wa kuvuka barabara, kuna magari, ila mara nyingi watu walio pembeni wa wakikuona umeshika hii fimbo wanatambua huoni wanakusaidia kuvuka.

"Nakutana na changamoto ikiwamo wakati wa kuvuka barabara, kuna magari, ila mara nyingi watu walio pembeni wa wakikuona umeshika hii fimbo wanatambua huoni wanakusaidia kuvuka.

"Ila kama si magari kufika sehemu nafika bila kuongozwa, nakariri zaidi, sauti, njia, hata mwendo wa hatua za mtu na hurufu pia. Mfano leo nimezungumza na wewe kesho sitakuuliza jina iwe kwa simu au tukionana njiani, ukiongea tu nitasema...shikamoo dada Christina.

"Hii hali tunayo wengi tulio hivi, akili lazima iwe kubwa sana kwenye kusikia, kukariri, ili ufike na ufanikiwe," anasema Regina.

**MSIMAMIZI WENYE ULEMAVU**

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama la Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), Ernest Kimaya, ana rai kwa serikali kupitia vyombo vya habari, akitala serikali iharakishe matumizi ya Daftari la Kudumu la Watu Wenye Ulemavu, kubaini idadi yao.

"Ili kila mmoja atambuliwe na kusajiliwa katika mtaa, kijiji wanapoishi kama inavyoelekeza Kifungu cha 23 cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu namba 9: 2010, daftari hili litasaidia," anasema Kimaya.

Pia anasema pendekezo la kundi lao kila wanapokutana ni kundi lao wawe katika mpango huduma za Mpango wa Watu Wenye Kaya Maskini (TASAF), kupewa mikopo ya asilimia mbili inayotolewa na halmashauri zote, ili wajishughulishe kiuchumi na kuwaondoa katika umaskini.

"SHIVYAWATA inawakumbusha waajiri wote kuzingatia ajira za watu wenye ulemavu, kwa uwiano wa asilimia tatu kwa mwajiri anayeajiri kuanzia watu 20 na kuendelea, kwa mujibu wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu," anasema Kimaya.

Anasisitiza, rai ya serikali na wadau kuwajengea uwezo wa kielimu kupitia vyuo vinavyotoa na stadi maalumu kwa wenye ulemavu, kwamba kutaibua vipaji na kuwapa msaada majumbani mwao, washiriki uzalishaji ili wao wajitegemee.

TANZIA

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# TUTAKUKOSA JOHN LIVETI

■Tunakukumbuka kwa falsafa ya unyenyekevu



John Liveti

HAKIKA siku zetu za kuishi zimehesababiwa na kwa mapenzi na neema yake Mungu hata leo tupo si kwamba tunastahili. Neno la Mungu linatuasa kuwa "tumshukuru Mungu kwa kila jambo".

Ninaandika haya nikimkumbuka mwandishi John Liveti ambaye kama ambavyo siku chache zilizopita; mauti ilimkuta rafiki, mwanatasnia na ndugu yetu Vedasto Msungu, aliyekuwa mtangazaji mahiri wa masuala mbalimbali ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira ITV na Redio One, ndivyo naye aliyetuacha.

Aliishi unyenyekevu na kila mara akiingia studio, alikumbusha kuwa falsafa ya ufagio ni unyenyekevu, licha ya kutumiwa kusafisha taka na popote haujawahi kususa kazi.

Imetokea ghafla kwa ndugu yetu John Liveti, akaaga dunia ghafla au kama ameugua ni kwa muda mfupi sana.

Tumempoteza mtangazaji mahiri katika tasnia ya habari aliyekuwa akitangaza katika televisheni ya Tumaini Media wamiliki wa Radio, Televisheni na Gazeti Tumainiletu.

Marehemu John Liveti alijiunga na Tumaini Media kama mtangazaji wa kawaida baada ya kumaliza mafunzo mwaka 2006.

Hadi mauti inamkuta hakuwahi kufanyakazi kwenye taasisi nyingine. Vilevile, kutokana na utumishi wake mzuri, mwaka 2015 aliteuliwa kuwa mkuu wa kitengo cha kuratibu matukio ya kikanisa, wajibu aliokuwanao hadi mwisho wa uhai wake.

Liveti alikuwa mtangazaji mzuri na mwenye kuipendakazi yake.

Amefariki Jumatano Machi 3, 2021 asubuhi. Nakumbuka mwanangu wa kwanza alikuwa akisikiliza kipindi cha "Hali Halisi" kinachorushwa na asubuhi na kusikia mchangia mada iliyokuwa inajadiliwa, akiwapa pole watangazaji wote na wanahabari kutokana na msiba wa Mtangazaji John Liveti wa Radio Tumaini maarufu Radio ya Ujirani.

Sikusikia wakati huo nilikuwa mbali na mahali alipokuwa amekaa akisikiliza matangazo hayo. Baada ya kusikia hivyo akaja akaniambia John hatunaye tena ameaga dunia. Nikashtuka na kusema: "What Liveti I know amekufa?" Hapohapo nikajawa na majonzi sana lakini nikajipa moyo kwa kutambua kuwa binadamu tu mali ya Mwenyezi Mungu ambaye ndiye mwenye mamlaka na hatimiliki juu ya uhai wetu.

Ni yeye peke yake anayeweza kuhuisha na kufisha hivyo tumshukuru Mungu kwa yote na jina lake lihimidiwe.

Tumempoteza mtangazaji mahiri katika tasnia ya habari aliyekuwa akitangaza na kujihusisha na masuala ya habari kupitia Radio, Televisheni Tumaini na Gazeti Tumaini Letu.

Kimsingi marehemu Liveti alikuwa mahiri na mwenye kuipenda kazi yake na alijitahidi kwa uwezo wake wote kutimiza wajibu kwa moyo wake wote. Kwa mara ya kwanza nilikuta na John Liveti mwaka 2013 katika eneo karibu na Tabata Shule.

Ni mahali ambapo mimi na familia nzima kulikutana na baadhi ya watumishi wa Tumaini Media kwa lengo la kufahamiana na kutakiana heri na fanaka kwa mwaka huo na miaka itakayofuata tukiongozwa na Mwenyezi Mungu.

Baada ya hapo tuliendelea kuwa pamoja katika masuala mbalimbali ya kiroho, kijamii pia kueneza elimu juu ya uhifadhi wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali zetu.

Vilevile, nimekuwa nikifuatilia baadhi ya vipindi alivyokuwa akivishughulikia mfano, kipindi cha "Miito" wakati akifanya mahojiano na watawa mbalimbali wa kike na wakiume. Kadhalika, nimekuwa namsikiliza akiendesha kipindi cha "Katekesi" akihojiana na mwalimu kutoka Parokia ya Magomeni na wakati mwingine huwa namsikia Gaudence Hyera akifanya mahojiano na mwalimu huyo lakini kwa nyakati tofauti.

**UNYENYEKEVU**

Hata hivyo, kilichokuwa ninanivutia kwa John Liveti ni kule kuwa na moyo wa unyenyekevu maana alipokuwa akianza kipindi lazima aseme yeye ni mdogo katika wadogo wote na kuongeza kuwa;

Falsafa ya ufagio ni 'unyenyekevu'." Hii ilikuwa ndiyo fimbo yake na ishara ya kujitambusha kuwa yeye ni nani katika jamii.

Hakika tumempoteza mnyenyekevu kati ya wanyenyekevu mbele ya Mwenyezi Mungu na binadamu pia. Mungu kwa mapenzi yake airehemu roho yake: "Raha ya milele umpe ee Bwana na Mwanga wa milele umwangazie; John Liveti apumzike kwa amani," Amina.

Pamoja na kushindwa kuhudhuria Misa ya kuuaga mwili wake lakini kiroho tulikuwa pamoja. Kusema kweli familia yangu nzima imehuzunishwa na kifo cha ghafla kwa ndugu yetu John Liveti.

Alikuwa kijana wa karibu na sisi na mara mbili au tatu aliungana nasi kwenye shughuli za kifamilia tukimshukuru Mungu nyumbani na pia kanisani.

Tunamshukuru sana kwa moyo wake wa upendo na kujituma pasipo shuruti hata kuweza kujumuika pamoja nasi na wengi wengi. Hatuna la kusema isipokuwa kutamka kuwa "Bwana alitoa sasa Bwana ametwaa Jina la Bwana Mungu wetu libarikiwe". Tuendelee kumwombea kwa Bwana Mungu wetu ili roho yake ipumzike kwa amani na kwamba, familia ya marehemu isichoke kumtegemea Mungu ambaye ndiye muweza wa yote. Shetani asiwashinde kiroho na kimwili.

Pole pia kwa wana-Tumaini Media wote, pamoja na wanahabari wote hapa nchini kwa kumpoteza mfanyakazi mwenzao.

Vilevile, pole kwa ndugu na jamaa wote walioguswa na msiba huu. Mwenyezi Mungu awajalie amani na upendo na kuyafanya yote kwa Utukufu wa Mungu.

Tunatambua kuwa tumempoteza mtangazaji na mwana habari mahiri lakini yote tumkabidhi Mungu Mwenyezi, ambaye kwa mapenzi na kwa neema yake sisi tunaishi. Hatujui saa wala siku lakini tuendelee kumuomba Mungu atutie nguvu na atujalie amani mioyoni mwetu pia atuwezeshe kuyatimiza mapenzi yake katika dunia hii iliyojaa machafuko na uovu wa kila namna.

Pamoja na hayo tujipe moyo maana tunayaweza yote kwa sababu yupo hai anayetutia nguvu na kwa uwezo wake tuweze kukesha kila wakati ili atakapokuja atukute tupo macho na taa zetu zinawaka huku zimejaa mafuta ili tuweze kumlaki kwa shangwe.

Hakuna lisilowezekana mbele za Mungu bali yote yawezeka kwake aaminiye na kutii na kiliishi neno lake wakati wote.

Tumshukuru Mungu kwa kila jambo na kumtolea dhabihu za shukrani zilizokamilifu kwa ajili ya utukufu wa jina lake Takatifu.



# Tume yaonya udhalilishaji mwanamke

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeitaka jamii kutofumbia macho matukio yenye kudhalilisha utu wa mwanamke na kutoa taarifa katika mamlaka husika.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu, Mathew Mwaimu, aliyasema hayo jana alipokuwa akitoa taarifa kwa vyombo vya habari katika Siku ya Wanawake Duniani ambayo iliadhimishwa jana.

Jaji Mwaimu alisema ni vyema jamii ikaachana na mitazamo potofu ya kumchukulia mwanamke kama chombo dhaifu kisichoweza kuleta matokeo chanya ya uongozi ili kujenga jamii yenye usawa.

“Kupitia jitihada mbalimbali za uhamasishaji zilizofanyika nchini kumekuwapo na ushiriki wa wanawake katika masuala ya uongozi kwenye vyama vya siasa, Serikali, Bunge, Mahakama na katika nafasi nyingine za uongozi katika jamii,’” alisema Mwaimu.

Alisema pamoja na jitihada mbalimbali za serikali za kukemea vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake bado kumekuwapo na tatizo hilo.

Alibainisha wanapowania nafasi za uongozi kumekuwapo na mila na desturi zinazomnyima haki za wanawake.

Mwaimu alisema serikali imeridhia mikataba na matamko mbalimbali ya kimataifa inayotoa haki kwa kila mtu kushiriki katika nafasi ya uongozi na utawala wa nchi kwa usawa wa kijinsia, Tume inaunga mkono dhamira hiyo ya serikali na kuwahamasisha wanawake kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

“Tume kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikiwahimiza wanawake kuendelea kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kuanzia ngazi za kijiji/mtaa hadi taifa na kuwajengea uwezo wa namna ya kudai haki zao kisheria pale wanapohisi haki hizo kuvunjwa,” alisema Mwaimu.

Jaji Mwaimu alisema kupitia kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu 2021 ambayo ni ‘Wanawake katika Uongozi, Chachu kufikia Dunia yenye Usawa’, Tume inaihamasisha jamii yote kuendelea kuchukua hatua madhubuti katika kuhakikisha kwamba ushiriki wa wanawake katika uongozi unaongezeka ili kufikia dunia yenye usawa.

# TAKUKURU yashtukia mifumo 24 ya utendaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma, imebaini mifumo 24 ya utendaji na utoaji wa huduma katika maeneo mbalimbali inayochangia vitendo vya rushwa.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa TAKUKURU mkoani humo, Sosthenes Kibwengo, alisema ofisi hiyo imefanya uchambuzi katika wilaya za Kondoa, Kongwa, Chemba,

Mpwapwa, Bahi na Chamwino kuanzia Julai mwaka jana na kubaini hayo.

**Mambo yanayochangia kuzorota kwa ukusanyaji wa ushuru yalibainishwa na maazimio ya kuboresha yametolewa.**

Alisema mifumo hiyo iliyofanyiwa uchambuzi ipo katika sekta za kodi, utawala, maji, afya, mikopo na ujenzi.

Aidha, Kibwengo alisema wamefanya uchambuzi wa mianya ya rushwa katika mfumo wa ukusanyaji wa ushuru wa huduma uliofanyika katika wilaya zote za mkoa huo.

“Mambo yanayochangia kuzorota kwa ukusanyaji wa ushuru yalibainishwa na maazimio ya kuboresha yametolewa,” alisema.

Kadhalika, alisema katika ufuatiliaji wa matokeo umeonyesha kwamba baadhi ya makandarasi wanaofanya miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji na barabara hawalipi kodi hiyo kwa halmashauri.

“Ushirikiano wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Mamlaka ya Majisafi na Mazingira Dodoma (DUWASA) na Halmashauri ya Jiji la Dodoma umewezesha kuwa na makubaliano ya wadau kushirikiana kuwaelimisha na kuwabana kimkataba makandarasi kulipa kodi hiyo,” alisema.

Alitoa wito kwa viongozi wa klabu za wapinga rushwa za vyuo vya elimu ya juu mkoani humo kuendelea kutoa elimu ya kupinga vitendo vya rushwa kwa kushirikiana na taasisi hiyo.




Baadhi ya watumishi wa umma wanawake wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakiwa katika maandamano ya Siku ya Wanawake kimkoa Machi 8, 2021 jijini Dodoma. **PICHA: UTUMISHI**

# Wanawake EWURA wapiga jeki watoto njiti

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WANAWAKE wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), wametoa kiasi cha Sh. milioni tano kwa ajili ya kununua vifaa tiba vya watoto njiti kwenye Kituo cha Afya Makole, jijini Dodoma.

Akikabidhi msaada huo kwa Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Mwenyekiti wa Wanawake wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE), tawi la EWURA, Herieth Kasilima, alisema katika kuadhimisha Siku ya Wanawake wameona watoe msaada huo ili kusaidia kuboresha huduma za afya.

“Niishukuru menejimenti ya wafanyakazi EWURA kwa kutoa msaada...naamini itakuwa faraja kwa wazazi wanaopata watoto njiti kupitia msaada huu watahudumiwa tunaamini fedha hii itanunua vifaa vinavyohitajika,” alisema.

Alisema msaada huo umetokana na kituo hicho kuwa na mpango wa kuanzisha huduma ya watoto njiti, hivyo fedha hiyo itasaidia kufanikisha mipango hiyo.

Aliishukuru Bodi ya Wakurugenzi EWURA kwa kuidhinisha kiasi hicho kitolewe na kukabidhiwa kwa kituo hicho ili kusaidia jamii hasa watoto wanaozaliwa katika kituo hicho na maeneo mengine watakaopelekwa katika kituo hicho.

Akipokea msaada huo, Kaimu Mganga Mfawidhi kituo hicho, Dk. Tumain Kapungu alishukuru kwa msaada huo kwa kuwa kituo hicho kimekuwa kikipata watoto wanaozaliwa kabla ya wakati.

“Tupo katika mchakato wa kukarabati wodi kwa ajili ya watoto njiti naamini msaada huu utachangia kwa kiasi kikubwa katika kununua vifaa kwa ajili ya wodi hiyo,” alisema.

Aliwaomba watumishi wa mashirika na taasisi nyingine kuona namna ya kujitolea kutoa misaada kama hiyo kwa sababu uhitaji bado upo.

“Vifaa vinavyohitajika katika wodi hiyo vinathamani ya Sh. milioni 27 pamoja na ukarabati wa wodi,” alisema.



# RC ataka EFD zitolewe kwa wafanyabiashara wote

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameishauri serikali kutoa mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFD) kwa wafanyabiashara wote nchini bila kujali kiwango cha mauzo ili kudhibiti ukwepaji kodi unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara kwa kutumia sheria zilizopo.

Alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki wakati alipokuwa anafungua mafunzo kwa maofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri za wilaya zote za mikoa ya Njombe na Katavi kuhusu usajili wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo ya kifedha yaliyoandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Aliishauri Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), kubadili mfumo wa ukadiriaji wa kodi kwa wafanyabiashara na kwamba ikiwezekana wasiwe wanatangaza viwango vya mauzo kwa mtu anayestahili kupata msamaha wa kodi.

Alisema kwa sasa sheria za kodi zilizopo zinaweka mianya ya wafanyabiashara kukwepa kodi kwa kuhakikisha mauzo yao hayazidi kiwango kinachotakiwa kulipa kodi.

**Kwa sasa kinachofanyika ni kutoa mafunzo kwa hawa viongozi ambao ndio wanaosajili hivi vikundi ili wanaposajili sheria na miongozo izingatiwe.**

Alisema Sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT) inatoa msamaha kwa mfanyabiashara ambaye mauzo hayafiki Sh. milioni 100 kwa mwaka na sheria ya matumizi ya mashine za EFD inatoa msamaha kwa mfanyabiashara ambaye mauzo hayazidi Sh. milioni 14 kwa mwaka.

"Sasa wafanyabiashara wanajitahidi mauzo yao yasifike Sh. milioni 14 kwa mwaka ili asipewe mashine hii na wengine wanajitahidi mauzo yasifike Sh. milioni 100 ili asiingizwe kwenye VAT, sasa nashauri ikiwezekana kila mfanyabiashara anayefanya biashara halali apewe mashine," alisema Chalamila.

Alisema idadi ya wafanyabiashara ambao wanafanya shughuli zao kiujanja ujanja ni wengi na kwamba njia pekee ya kuwadhibiti ni kuhakikisha wanapewa mashine wote bila kujali viwango vya mauzo.

Mkurugenzi wa BoT tawi la Mbeya, Ibrahim Malogoi, alisema benki hiyo inaendelea na taratibu mbalimbali za usajili wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo ya fedha nchini.

Alisema moja kati ya maandalizi ambayo tayari yamefanyika ni pamoja na kutunga kanuni za usimamizi wa huduma hiyo kwa kila ngazi ya vikundi pamoja na kufanya tathmini ya mamlaka ambazo zimekasimiwa kwa vikundi hivyo.

Vilevile, alisema wameandaa mifumo na miongozo ya usajili wa watoa huduma hao wa pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu sera na sheria ya usimamizi wa huduma ndogo ya fedha.

Baadhi ya Maofisa Maendeleo ya Jamii walioshiriki mafunzo hayo, waliahidi kuhakikisha vikundi vyote vya kijamii vya huduma ndogo ya fedha ambavyo ni pamoja na Vyama vya Kuweka na Kukopa (SACCOS) na Vikoba vinavyoundwa katika maeneo yao vinasajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Mmoja wa maofisa hao, Julius Mwakajila aliwaomba maofisa wa BoT kuendelea kutoa mafunzo hayo ili wafanye kazi kwa ustadi na kuhakikisha sheria zinazingatiwa.

## Wasomi vyuo vikuu watakiwa kutetea maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WASOMI wa vyuo vikuu nchini, wametakiwa kutumia elimu yao kulinda rasilimali za nchi pamoja na kutetea maendeleo ya taifa ili kudumisha uzalendo na kuiwezesha serikali kufikia malengo ya taifa.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo, alisema hayo wakati alipokuwa anatoa elimu ya itikadi na uongozi wa kwa makada wa chama hicho wa Tawi la Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST).

Alisema serikali imefanya mambo mengi ya maendeleo, lakini wakati mwingine mambo hayo hayajulikani kutokana na kukosa watu wa kuyatangaza vyema kwa wananchi na kuwataka vijana hao kuwa sehemu ya kueneza habari hizo njema.

Dk. Mwakajumilo aliwataka vijana hao kuwa tayari hata kupigana kwa ajili ya kulinda rasilimali za nchi ambazo wakati mwingine huwa zinamendewa na mabeberu.

"Tunapolinda maslahi ya taifa sio kwamba tunamlinda tu Rais wetu Dk. John Magufuli bali tunakuwa tunalinda taifa letu, sasa moja kati ya jukumu letu sisi makada wa CCM ni kulinda taifa," alisema Dk. Mwakajumilo.

Mwenyekiti wa CCM Seneti ya vyuo vikuu Mkoa wa Mbeya, Halima Magumba, alisema vijana ndio nguzo ya chama na mwanzo wa kuzalisha viongozi bora na kuwataka wanachama wenzake wa chama hicho kuisaidia serikali.



Madereva wa magari ya serikali wakilifanyia marekebisho gari la Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia watu wenye ulemavu, Ummy Nderiananga, wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevya, mkoani Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wapewa mafunzo utunzaji sahihi wa mafuta

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya wazalishaji na wafanyabiashara wa mafuta ya kupikia 490 katika mikoa ya Mbeya na Songwe, wamepatiwa mafunzo maalumu ya utunzaji sahihi wa bidhaa hiyo ili kuhakikisha inabaki na ubora wake.

Mafunzo hayo yaliyotolewa na Shirika la Viwango nchini (TBS), ni pamoja na kuepuka kuuza bidhaa hiyo wakiwa wameiweka juani ili kuepuka kuharibu ubora wake na kusababisha madhara kwa watumiaji.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Uhusiano wa TBS, Roida Andusamile, alisema walikuwa wanatoa mafunzo hayo kwa kila halmashauri kwa kuanzia na za Mkoa wa Mbeya na wahusika walikuwa ni wazalishaji wa mafuta na wauzaji.

Alisema katika Mkoa wa Mbeya, walitoa mafunzo hayo kwenye Halmashauri za Mbeya ambako washiriki walikuwa 94, Kyela (101), Rungwe (62) na Chunya washiriki (62).

Alisema kwa Mkoa wa Songwe mafunzo hayo yalitolewa katika halmashauri mbili za mji wa Tunduma na Mbozi na katika Mji wa Tunduma washiriki walikuwa 61 na Mbozi 119.

"Sisi kama wasimamizi tumeona ni muhimu kuonana na hawa wadau katika maeneo mbalimbali ili wapate elimu, hawa wachache waliohudhuria mafunzo haya watakuwa mabalozi huko mitaani kwa kuwaelimisha wenzao," alisema Andusamile.

Alisema maofisa wa TBS waligawanyika katika makundi mawili, Iringa na Njombe na wengine Mbeya na Songwe ili kuhakikisha kazi hiyo inafanyika kwa haraka na ufasaha.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Hamis Mwanasala, alisema mafunzo hayo yalilenga zaidi kuwaelimisha wafanyabiashara kuhusu kuacha tabia ya kuanika mafuta juani kwa maelezo kuwa utaratibu huo unaharibu ubora wa mafuta.

Alisema pia kuna hatari bidhaa hiyo ikasababisha madhara ya kiafya kwa watumiaji wa bidhaa hiyo ikiwa imepoteza ubora.

Vilevile, aliwataka wadau hao kuandaa bidhaa hiyo katika mazingira ya usafi ili kulinda afya za watumiaji kwa kuwa watumiaji wa bidhaa hiyo nchini ni wengi.

"Pia tumetoa elimu juu ya ufungashaji bora na uwekaji wa taarifa muhimu kwenye vifungashio, usajili wa bidhaa na majengo ya kuzalishia na kuhifadhia kama sheria inavyotaka," alisema Mwanasala.

Mwanasala alisema baadhi ya kazi ambazo shirika hilo linafanya zilikuwa zinafanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa na vifaa tiba (TMDA).





## Changamoto zinazokabili wanawake zatajwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman, amesema pamoja na juhudi mbalimbali zinazochukuliwa katika kuhakikisha wanashiriki katika maamuzi na uongozi, bado zipo changamoto zinazorudisha nyuma maendeleo ya wanawake.

Aliyasema hayo wakati akizungumza katika kongamano la maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani lililofanyika katika ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdula Wakil, Kikwajuni Mjini Zanzibar.

Alisema baadhi ya changamoto hizo ni kuwapo kwa mifumo dume ndani ya vyama vya siasa isiyotoa kipaumbele kwa wanawake kushika nafasi za uongozi na kusababisha ushiriki wa wanawake kuwa mdogo na kukosekana kwa usawa baina ya wanaume na wanawake katika nafasi za uongozi.

Alisema changamoto nyingine ni kuwapo kwa mifumo ya malezi ya watoto ndani ya jamiii isiyojenga uthubutu wa kujiamini kwa mtoto mwanamke pamoja na kuwapo kwa mfumo dume unaompa kipaumbele mwanaume na kujenga fikra potofu dhidi ya mwanamke.

Alisema uwezo mdogo wa kiuchumi unaowakabili wanawake wengi Zanzibar ni kikwazo kingine kinachosababisha wanawake kushindwa kushiriki katika mchakato wa kugombania nafasi mbalimbali za uongozi.

"Kadhalika baadhi ya wanawake wanaojitokeza katika kugombania nafasi mbalimbali hukumbwa na vitendo vya udhalilishaji suala ambalo huwapelekea baadhi yao kukata tama," alisema.

Aidha, alisema Serikali ya Zanzibar, itazifanyia kazi changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake na itaendelea kuzingatia masuala ya kijinsia wakati wa uteuzi wa watendaji mbalimbali kushika nafasi za uongozi.

# Tani 20 dawa zinazodaiwa kuwa bandia kuteketezwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar, inatarajia kuangamiza tani zaidi ya 20 ya dawa mbalimbali bandia zilizoingizwa nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Mkurugenzi wa Idara ya Dawa na Vipodozi ya mamlaka hiyo, Bora Mposanje Lichanda, alisema dawa hizo zimeingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

Alisema kuwa dawa hizo hazifai kwa matumizi ya binadamu kutokana na kutokua na ubora.

Pia alisema usalama na ubora wa dawa hizo unatia mashaka na hazifai kutumiwa na binadamu kwa sababu zinaweza kuleta athari.

**Dawa hizo zimeingizwa nchini mwezi uliopita na alisema mmiliki wa dawa hizo atatakiwa kulipa faini au kupelekwa mahakamani kwa mujibu wa sheria.**

Dawa hizo zimeingizwa nchini mwezi uliopita na alisema mmiliki wa dawa hizo atatakiwa kulipa faini au kupelekwa mahakamani kwa mujibu wa sheria.

"Hiki ni kiwango kikubwa sana cha dawa ambazo tumezikamata kwa mwaka huu na dawa hizi zimeshaanza kuuzwa katika maduka ya dawa ambapo dawa hizi ni kwa ajili ya kutibu kifua na mambo mengine," alisema.

Akizungumzia kuhusu athari za kimazingira kwa kuangamizwa kwa dawa hizo, alisema athari lazima zitakuwapo, lakini kwa kuwa hawana kiwanda maalum kwa ajili ya kuangamiza dawa, wanasubiri maelekezo kutoka kwa wataalamu wa mazingira.

Akizungumza na Nipashe mfanyabiashara aliyeingiza dawa hizo, Ali Ahmed, alisema dawa hizo sio bandia isipokuwa zimekosekana jina la kiwanda kilichotengeneza, pia waliingiza mzigo huo kisheria na kuthibitishwa kuingiza nchini.

"Kama dawa hizo ni feki wazipeleke maabara, lakini kwanini ziliruhusiwa kuingia na kupita bandarini mimi nadhani wao wenyewe bodi ya chakula hawapo makini," alisema Ahmed.



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi, akikabidhiwa Taarifa ya Utekelezaji wa Mradi wa Amka Mwanangu Soma kwa Bidii wa Jumuiya ya Rafiki wa Wanawake na Watoto Zanzibar (RAWWAZA) na Mshika Fedha wa Taasisi hiyo, Valeria Rashid Haroub. Hafla hiyo ilifanyika jijini hapa juzi. **PICHA: IKULU**

# Waziri aanika vipaumbele kuwainua wanawake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohamed Mussa, amesema wanawake wanahitaji kupewa kipaumbele katika kuwezeshwa kielimu, kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Alisema mambo hayo yanahitaji kushughulikiwa kwa haraka kwa ujenzi wa taifa lenye uhakika na mafanikio kupelekea Zanzibar ya uchumi wa bluu.

Aliyasema hayo baada ya kumaliza matembezi ya hiari katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani yaliyoadhimishwa na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), viwanja vya Mwenge Mwanakwerekwe.

Alisema jamii isipochukua jitihada za madhubuti za kuthamini na kuheshimu mchango wa mwanamke kama ni nguvu makini kwa maendeleo endelevu, itapata madhara hasa kwa vile wanawake ni wazalishaji wakuu.

Alisema kuwa madhara ni pamoja na kuwapo kwa idadi kubwa ya wanawake kukosa haki zao za msingi, kuongezeka kwa unyanyapaa kwa wanawake na utelekezaji, kuongezeka kwa umaskini na kupungua kwa ajira na kipato kwa wanawake.

"Matukio yote haya yanaenda kinyume na sera ya maendeleo ya wanawake ya mwaka 2016, hivyo ni jukumu letu sote kuweka mikakati ya kuhakikisha wanawake wote bila kujali hali zao wanapata haki zao za msingi zinazohitajika kwa ajili ya kuleta maendeleo chanya katika uchumi wa bluu," alisema.

Alisema kuwa jukumu la kuhakikisha kuwa wanawake wanakuwa katika uchumi wa buluu na kupata haki zao ni la jamii nzima. Kila mmoja alisema anatakiwa kutekeleza jukumu hilo kwa uhakika lengo ni wanawake wanawezeshwa kushiriki katika michakato ya shughuli za maendeleo endelevu kwa wananchi katika sekta za kiuchumi na kijamii.

Aliwataka kudumisha amani na haki ya usawa kwa kila binadamu bila kujali tofauti zao.

Akisoma risala ya Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar, mmoja wa wanachama a jumuiya hiyo, Rukia Mkali, alisema imepambana na changamoto mbalimbali katika kuhakikisha wanawake wanapata haki zao kwa kutoa msaada wa kisheria na mambo mengine yanayowahusu wanawake na watoto.

## HABARI KIMATAIFA

# Mke wa Prince Harry asimulia machungu

**Washington, MAREKANI**

MKE wa mwanamfalme Harry, Meghan Markle, amesema alipitia maisha magumu sana katika familia ya kifalme, akisema hakutaka tena kuwa hai.

Katika mahojiano ya kibinafsi na hisia kali kupitia televisheni, Meghan alimwambia mtangazaji Oprah Winfrey, kwamba hakupata usaidizi wakati alipouhitaji.

Alisema kibaya zaidi ilikuwa mmoja wa familia hiyo alipomuuliza mumewe, Harry, jinsi mtoto watakayemzaa atakuwa na ngozi nyeusi.

Prince Harry pia alifichua kwamba babake Prince Charles aliacha kuzipokea simu zake, alipogundua kwamba alikuwa na mpango wa kujiondoa kutoka familia ya kifalme.

Mahojiano hayo na Oprah yaliyongojewa sana yalipeperushwa usiku nchini humo.

Oprah alimuuliza: "Kwamba hutaki kuishi tena?" "Ndio," Meghan alithibitisha.

Wakati wa mahojiano hayo maalum ya CBS ya saa mbili ambayo yatapeperushwa jana usiku katika runinga ya ITV nchini Uingereza, pia kwenye ITV Hub kwa hisani ya Harpo Productions/CBS, wanandoa hao walizungumzia masuala mbalimbali, ikiwamo ubaguzi wa rangi.

Pia walizungumzia uhusiano wao na vyombo vya habari, afya ya akili na mambo mengine katika familia ya kifalme.

Kadhalika kwenye mahojiano hayo walitangaza kuwa wanatarajia kupata mtoto wa kike hivi karibuni.

Wakati wa mahojiano hayo, familia ya kifalme ilishtumiwa kwa kukosa kuwaliwaza Harry na mkewe, huku Meghan akisema hali ilianza kuwa mbaya baada ya kuoana, Mei mwaka 2018.

Prince Harry na Meghan, walihamia California, baada ya kujitoa kutoka katika majukumu ya familia ya kifalme Machi mwaka jana na ilitangazwa mwezi uliopita kwamba hawatarejea kama wanachama wa familia ya kifalme.

Harry alizungumzia uhusiano wake na watu wengine wa familia ya kifalme na kwamba yeye na bibi yake, Malkia Elizabeth, uhusiano wao ulikuwa mzuri sana.

Hata hivyo alisema uhusiano kati yake na baba yake, Mwanamfalme Charles wa Wales, umevurugika.

Harry alisema anahisi kufelishwa na kwamba ataendelea kumpenda ingawa kuna kuumizwa kwingi.

Kukusu kaka yake, Mwanamfalme William alisema wapo katika njia tofauti, pia alifichua kwamba familia yake ilikuwa imekoma kumpa msaada wa kifedha.

**BBC**




Papa Francis akipanda ndege baada ya kumaliza ziara yake ya siku nne nchini Iraq, katika Uwanja wa Ndege wa Baghdad, jana. **PICHA/AP**

# Watu 15 wafariki katika mlipuko

**Bata, EQUATORIAL GUINEA**

WATU takriban 15 wamefariki dunia huku wengine zaidi ya 100 wakipata majeraha katika mfululizo wa milipuko iliyotokea nchini Equatorial Guinea, Wizara ya Afya imesema.

Baadhi ya watu 500 walijeruhiwa kufuatia milipuko hiyo iliyotokea karibu na kambi za wanajeshi mji mkuu wa Bata Jumapili.

Milipuko hiyo ilisababishwa na uzembe uliohusishwa na hifadhi ya baruti kali kambini.

Picha kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha moshi mkubwa na uharibifu uliotokea.

Televisheni inayomilikiwa na serikali ilionyesha watu wakitafuta manusura katika vifusi huku wakiinua vipande vya majengo yaliyoporomoka.

Rais Teodoro Obiang Nguema, alisema katika taarifa kwamba athari iliyotokana na mlipuko huo ni uharibifu mkubwa karibu nyumba zote na majengo huko Bata, na kutoa wito wa usaidizi wa kimataifa. Aliongeza kwamba huenda tukio hilo limetokea kufuatia hatua ya wakulima kuchoma mashamba yanayozunguka kambi za jeshi.

Katika mfululizo wa ujumbe uliotumwa kwenye mtandao wa Twitter, waziri wa afya aliomba wahudumu wa afya kujitolea na kwenda katika hospitali ya eneo la Bata.

Pia ilitoa wito watu kujitolea kutoa damu kwa sababu ya idadi kubwa ya waliojeruhiwa na iliorodhesha hospitali tatu ambazo waliojeruhiwa zaidi watapelekwa.

Baadhi ya hospitali za eneo hilo zilipokea wagonjwa kupita kiasi, TVGE iliripoti.

Televisheni hiyo ilionesha picha za watu waliojeruhiwa wakiwa wamelala kwenyesakafuyahospitalimoja iliyojaa watu.

"Tumesikia mlipuko na sasa tunaona moshi, lakini hatujui kinachoendelea," mkaazi mmoja wa eneo amezungumza na Shirika la Habari la AFP.Katika mtandao wa Twitter, Balozi wa Ufaransa, Olivier Brochenin alituma risala za rambirambi kwa waathirika, akizungumzia ajali hiyo kama "janga".

Ubalozi wa Uhispania ulisema kuwa, raia wa nchi yake wasalie nyumbani na kutoa namba kadhaa za simu za dharura.

Equatorial Guinea, ilitawaliwa na Uhispania hadi ilipojipatia uhuru wake mwaka 1968.

**BBC**

## Boti yenye shehena mafuta yakwama Mauritius

**Port Louis. MAURITIUS**

BOTI ya uvuvi iliyo na bendera ya China, imekwama katika miamba ya matumbawe nchini Mauritius, karibu kilomita 10 kutoka mji mkuu wa Port Louis.

Chombo hicho, kiitwacho LURONGYUANYU 588, kilikwama Pointe aux Sables, maili chache kutoka ufukweni.

Ilikuwa imebeba tani 130 za mafuta ya dizeli na tani tano za mafuta mengine ingawa haikuwa na samaki, kulingana na Waziri wa Uvuvi, Sudheer Maudhoo.

Boti hiyo ilikuwa imepangiwa kuhamisha mafuta kutoka kwenye meli na kuchukua.

"Kwa sasa inaelea juu ya maji na hakuna mafuta yaliyomwagika kufikia sasa," waziri alisema.

"Mipango ya dharura imefanywa endapo mafuta yataanza kumwagika kutoka katika chombo hicho Bandari ya Port Louis."

Wafanyakazi 16 wa boti hiyo waliokolewa juzi jioni, walikuwa raia 14 wa China baharia mmoja raia wa Indonesia na mwingine wa Ufilipino.

Walinzi wa kitaifa wa pwani ya Mauritius walisema walipokea ombi la msaada kutoka kwa boti hiyo ya uvuvi.

Bahari ikiwa na dhoruba ilifanya operesheni ya uokoaji kuwa mgumu hadi helikopta ya polisi ilipoitwa.

**BBC**

## Kesi mauaji George Floyd yaanza

**Minneapolis, MAREKANI**

KESI ya ofisa anayedaiwa kusababisha kifo cha George Floyd, Mmarekani mweusi, baada ya kukandamizwa kwa goti shingoni na mgongoni huko Minneapolis, Mei 25, imeanza jana.

Geoge Floyd (46) alifariki baada ya ofisa wa polisi mzungu kumwekea goti lake katika shingo yake kwa zaidi ya dakika nane.

Kesi ya Ofisa wa Polisi, Derek Chauvin ilianza jana huko Minneapolis ambaye anahusishwa kwa kosa la mauaji.

Kwa mujibu wa uchunguzi binafsi wa maiti yake, George Floyd, ambaye kifo chake kilisababisha maandamano makubwa Marekani, alikufa kutokana na ukosefu wa hewa safi ya oksijeni.

Alifariki kwa kukandamizwa kwa goti shingoni na mgongoni na maofisa wa polisi wa Minneapolis, uchunguzi wa kimatibabu uliosimamiwa na familia ya Floyd, ulibaini hilo.

Matokeo hayo yanatofautiana na matokeo ya uchunguzi wa mwili wake uliofanywa na madaktari wa kaunti.

Kulingana na matokeo hayo, hakukupatikana ushahidi wowote unaohusisha ukosefu wa hewa wala kunyongwa. **RFI**

## HABARI MICHEZO



# KLOPP

## SASA AJIPANGA KUPIGANIA NNE BORA

**LIVERPOOL England**

JURGEN Klopp amesisitiza Liverpool haitaacha kamwe kutafuta nafasi kwenye nne bora katika Ligi Kuu England ili kupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Liverpool ambao ni mabingwa watetezi wa taji la Ligi Kuu England, iliweka rekodi mpya Jumapili walipofungwa 1-0 na Fulham na kushuka hadi nafasi ya 8 kwenye msimamo.

Shambulizi la Mario Lemina kabla ya mapumziko pale kwenye dimba la Anfield lilishuhudia 'Wekundu' hao wakipoteza kwa mara nyingine.

Liverpool imekuwa katika msimu mgumu tangu kuanza kwa mwaka mpya, ikiwa na ushindi mara tatu tu kwenye ligi katika michezo 13, ikiwaacha wakipoteza kwa timu za nne bora.

Kwa mara ya kwanza katika historia yao, klabu hiyo ya Merseyside ilikubali bao la ufunguzi wa mchezo mara sita mfululizo nyumbani.

Liverpool walikuwa wamepoteza kwa Burnley, Brighton, Manchester City, Everton na Chelsea kwenye ardhi ya nyumbani kuelekea mechi ya Jumapili, ikikubali kipigo cha bao moja pekee.

"Siwezi kufikiria juu ya kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwani tunapaswa kupitia raundi hii ngumu," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Liverpool ni kubwa mno, watu wengi wanavutiwa. Hatuchezi nyuma ya milango iliyofungwa bila kamera, iko mbele ya watu wetu na tunahisi jukumu kwamba katika kila mchezo tunapaswa kutoa kila kitu chetu kushinda.

"Ikiwa hilo halitatokea basi watu watafikiria," hiyo haitoshi. "Hatubadilishi mtazamo wetu." Aliongeza Klopp.

"Kwa namna yoyote lazima tupambane kumaliza kwenye nne bora, maana hali kwetu kwa sasa ni ngumu mno, tukishindwa kufanya hivyo maana yake tutaendelea kuwa vibaya na vibaya zaidi."

# Laporta ashinda tena urais Barca

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa zamani wa Klabu ya Barcelona mwaka 2003 hadi 2010, Joan Laporta ameshinda tena nafasi hiyo kwa mara ya pili, katika uchaguzi wa urais uliofanyika juzi Jumapili.

Laporta ambaye moja ya sera zake ilikuwa ni kuhakikisha nyota na gwiji wa klabu hiyo, Lionel Messi, anabaki klabuni hapo, ameshinda kwa zaidi ya asilimia 54 ya kura zote.

Rais huyo mwenye umri wa miaka 58, aliwashinda wagombe wengine, Victor Font (asilimia 29.99) na Toni Freixa (asilimia 8.58) na kupata nafasi hiyo kwa mara ya pili kuiongoza tena Barca.

Laporta wakati akiwa rais kwa mara ya kwanza ndani ya klabu hiyo, alifanikisha usajili wa Ronaldinho Gaucho, na pia alimwajiri Pep Guardiola kuwa kocha wa klabu hiyo.

Amechekua nafasi ya Josep Maria Bartomeu ambaye alijiuzulu Oktoba mwaka jana.



# De Bruyne atoa sababu kuondoka Chelsea



**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa Manchester City, Kelvin de Bruyne, amekiri kwamba, aliamua kuondoka katika klabu ya Chelsea ili kuweza kupata nafasi ya kucheza zaidi.

De Bruyne amesema kwamba, hakupewa nafasi ya kutosha na alionekana kama asiyekuwa na mchango kwenye kikosi hicho.

"Niliamua kuondoka kwa sababu nilihisi sikuwa na nafasi yoyote ya kucheza wakati ule," alisema De Bruyne akiiambia Sky Sports juu ya sababu zake za kuondoka Chelsea

"Sikuona fursa zaidi zinakuja kwangu, ulikuwa uamuzi bora kuondoka Chelsea na kwenda katika hali ambayo nilihisi ningeweza kuanza tena.

"Je! Nilitarajia kwenda hivi? Ukweli sio, kwa sababu wakati huo nilikuwa na kiwango cha chini, lakini sikuwa na shaka yoyote juu ya uwezo wangu kama mchezaji wa mpira.

"Siwezi kufikiria ni nini kitatokea miaka minane chini ya safu ya kucheza kwa Manchester City, kwenye Kombe la Dunia na vitu vyote. Ni nzuri." aliongeza De Bruyne.

# XAVI ASHINDA TAJI LA KWANZA KAMA KOCHA

**DOHA, Qatar**

XAVI Hernandez amesherehekea taji lake la kwanza la Ligi Kuu akiwa kocha katika Klabu ya Al Sadd Jumapili, wakati timu hiyo ilipolibeba Kombe la Kuu ya nchini Qatar na anatarajiwa kurudi kuinoa Barcelona.

• Kiungo huyo wa zamani wa Hispania na Barca alishuhudia wachezaji wake wakibeba taji hilo baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Umm Salal na kuwafanya waongoze kwa tofauti ya pointi 13 huku zikiwa zimebaki mechi nne ligi kufikia tamati.

Xavi awali aliisaidia Al Sadd kushinda taji hilo msimu wa 2018-19 akiwa mchezaji, wakati akicheza mwaka wake wa mwisho kabla ya kustaafu soka.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 41, aliingia kwenye kazi ya ukocha mwaka uliofuata na ameisaidia Al Sadd kutwaa taji hilo.

"Tumetengeneza historia mpya kwa Al Sadd," alisema Xavi. "Nina furaha kushinda taji la ligi kwa mara ya kwanza kama kocha nikiwa na Al Sadd, baada ya kushinda kama mchezaji."

Mabao kutoka kwa Baghdad Bounedjah, Yousuf Abdurisag na Rodrigo Tabata yalilihakikishia timu hiyo ushindi huo.

Xavi aliiambia tovuti ya klabu hiyo: "Nina furaha kuwa kwenye kundi hili la wachezaji, maofisa, benchi la ufundi na timu ya madaktari. Malengo yetu ni kushinda kila mashindano tunayoingia."

# IBRAHIMOVIC YUPO TAYARI KUBAKI MILAN

**MILAN, Italia**

ZLATAN Ibrahimovic amesema yupo tayari kuongeza mkataba mpya na AC Milan kama Mkurugenzi wa Ufundi, Paolo Maldini "anataka."

Ibrahimovic amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia tangu aliporudi tena Milan kwa mara ya kwanza Januari mwaka jana, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39, ameiwezesha klabu hiyo kuwa kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A msimu huu.

Nyota huyo wa zamani wa Manchester United na Paris Saint-Germain - mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, amefunga mabao 14 kwenye Serie A na kuiweka Milan nafasi ya pili wakipitwa na Inter Milan.

Alipoulizwa kuhusu majaliwa yake, Ibrahimovic alisema: "Sijui, ngoja tuone. Kama Paolo anataka.

"Msimu huu bado ni mrefu, kuna mechi nyingi zimebaki.

"Mara zote tunacheza kushinda, hata kama wanaweza kucheza mara moja kwa wiki."



# BALE: SIWEZI KUCHEZA KAMA NINA MIAKA 21

**LONDON, England**

GARETH Bale hana uhakika kama anaweza kurudi kwenye kiwango alichokuwa nacho wakati wa kipindi chake cha kwanza kuichezea Tottenham Hotspur, licha ya kufurahia kufunga mara kwa mara.

Bale amefunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho tatu katika mechi sita zilizopita kwenye mashindano yote, akicheza kwa dakika 70 au chini yake kwa mechi zote hizo za ugenini.

Bale alikuwa kwenye orodha ya wafungaji kwenye mchezo wa ushindi wa Jumapili wakati wakichapa Crystal Palace 4-1.

Lakini alipoulizwa kama mashabiki wa Spurs wamtarajie kurudi kwenye kiwango chake kama cha msimu wa 2012-13 wakati alipohusika kwenye mabao 37 katika mechi 44, na kumfanya asajiliwe kule Madrid, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 alionyesha kusita.

"Muda utasema," alisema Bale akiiambia Sky Sports. "Sina umri wa miaka 21 tena. Ilikuwa kipindi kile.

"Nitaendelea kujituma na kucheza kwa bidii katika kila mchezo, kuuchukulia mchezo kwa umakini mkubwa na kuweza kufunga.

"Mwili unabadilika kutokana na muda. Huwezi kucheza kama ulivyokuwa kijana, kwa sasa mambo yamebadilika."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FERNANDES AFUNGUKA MAZITO PENALTI UNITED

Watasema hafungi katika mchezo wa wazi, ilikuwa ni penalti lakini jambo la muhimu kwetu ni kushinda...

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Manchester United, Bruno Fernandes amesisitiza "watu mara zote wanalalamika kuhusu kila kitu", kauli hiyo akiitoa baada ya kufunga kwenye mchezo wa 'dabi' wa Ligi Kuu England dhidi ya vinara, Manchester City.

Fernandes alifunga bao ndani ya sekundi 101 kwenye mchezo huo wa Jumapili kwa mkwaju wa penalti wakati Man United ikiibuka na ushindi wa 2-0, pale kwenye dimba la Etihad.

Ushindi huo wa Man United ulihitimisha umwamba wa Man City wa kushinda mechi 21 mfululizo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno alikuwa akishutumiwa kutokana na rekodi yake ya kushindwa kufunga dhidi ya timu sita za juu za ligi, hasa kiwango alichokionyesha kwenye mchezo wa Chelsea ambao ulimalizika kwa sare tasa.

Tottenham ndio ilikuwa timu pekee katika sita za juu ambayo Fernandes aliifunga bao msimu huu, akifunga kwa mkwaju wa penalti Oktoba mwaka jana, wakati walipochezea kichapo cha mabao 6-1.

"Kila penalti ina presha ile ile kwangu mimi," alisema Fernandes, ambaye amefunga mabao 16 na pasi za mwisho 10 kwenye mechi 28 za Ligi Kuu msimu huu, akiiambia MUTV wakati alipoulizwa namna alivyojisikia.

"Mara zote nakuwa na presha kubwa na penalti, haijalishi ni dhidi ya City, au timu nyingine yoyote. Mara zote nakuwa na presha kubwa kupiga penalti.

"Naipenda aina ile ya presha. Ni presha nzuri. Nilijua nini natakiwa kufanya. Nilifanya kwa muda muafaka na kwa nguvu kubwa na nina furaha kubwa kufunga, bila shaka yoyote.

"Kiukweli sisi tunachoangalia ni kushinda. Watu mara zote watalaumu kila kitu. Leo (juzi) watasema tena Bruno hafungi kwenye mechi kubwa.

"Watasema hafungi 'katika mchezo wa wazi, ilikuwa ni penalti na hatuihesabii! Lakini kwetu sisi jambo la muhimu ni kushinda mechi.

"Haijalishi unafunga kwa namna gani, wakati mpira ukigusa nyavu ni bao. Nitakuwa na furaha na sitajali nimefunga mimi au kafunga mwingine."

Luke Shaw alifunga bao la pili dakika tano baada ya mapumziko na United waliendeleza rekodi yao ya kutofungwa ugenini na kufikisha mechi 22.

Lakini United bado imepitwa pointi 11 na City waliopo kileleni, huku zikiwa zimebakia mechi 10 ligi kumalizika.

## KWA UFUPI

**SALAH AUZWE TU - FOWLER**

LIVERPOOL inapaswa kumuuza mshambuliaji wake, Mohammed Salah, mwenye umri wa miaka 28 raia wa Misri iwapo hafurahii kuwa hapo, kwa mujibu wa nahodha wa zamani wa klabu hiyo, Robbie Fowler. ***(Mirror)***

**XAVI ABEBA KOMBE LA KWANZA**

KIUNGO wa zamani wa Barcelona, Xavi Hernandez, ametwaa taji la kwanza kama kocha, baada ya kuiongoza Al Sadd kubeba Kombe la Ligi Kuu Qatar maarufu kama QNB Stars League. ***(Marca)***

**GERRARD HAONDOKI RENGERS**

MWENYEKITI wa zamani wa Rangers, Dave King, amesisitiza hakuna nafasi kwa kocha Steven Gerrard kuondoka hapo Ibrox na kwenda kuwa kocha mpya wa Liverpool kwa siku za hivi karibuni. ***(Glasgow Times)***

**DESCHAMPS AMTETEA GRIEZMANN**

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps, amesema haitakuwa sawa kuhoji nafasi ya mshambuliaji wa Barcelona, Antoine Griezmann kwenye kikosi cha timu ya taifa. ***(beIn Sports)***

**MOYES KUPEWA MKATABA**

WEST Ham inapanga kufanya mazungumzo na kocha wake, David Moyes ili asaini mkataba wa muda mrefu, baada ya uvumi kudai kwamba anawaniwa na klabu nyingine. ***(Teamtalk)***

**LIVERPOOL KUPOTEZA MMOJA**

NI jambo "lisiloepukika" kwa Liverpool kumpoteza mmoja kati ya washambuliaji wake watatu wa mbele na Salah, akiwamo Msenegal Sadio Mane mwenye umri wa miaka 28, au Roberto Firmino raia wa Brazil mwenye umri wa miaka 29, kipindi kinachokuja cha majira ya joto, amesema straika wa zamani wa Ireland, Tony Cascarino. ***(Talksport)***

**CHRISTENSEN NA MKATABA MPYA**

CHELSE inapanga kutoa ofa ya mkataba mpya kwa mlinzi wa Denmark, Andreas Christensen mwenye umri wa miaka 24. (Telegraph)

**MCCORMICK ATAKIWA MILLWALL**

KIUNGO wa Klabu ya Chelsea, Luke McCormick mwenye umri wa miaka 22, anatakiwa na Millwall ya Ligi Daraja la Kwanza. ***(Sun)***

**WOLVES YAMFUATILIA BROWNHILL**

KLABU za Wolves, Southampton, Crystal Palace, West Ham na Aston Villa zimekuwa zikimfuatilia kiungo wa Burnley, Josh Brownhill, mwenye umri wa miaka 25, katika miezi ya hivi karibuni. ***(Teamtalk)***

**IBRAHIMOVIC KURUDI SWEDEN**

STRAIKA wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 39, anapanga kurudi kuichezea timu ya taifa na anatarajiwa kuitwa kwenye kikosi cha Sweden mwezi huu. ***(Fotboll-Direkt, via Mail)***

**HAMSIK KUTUA GOTHENBURG**

KIUNGO wa zamani wa Lazio, Marek Hamsik mwenye umri wa miaka 33, anapanaga kujiunga na IFK Gothenburg. Raia huyo wa Slovakia amekuwa akicheza kwenye Ligi Kuu China katika Klabu ya Dalian Professional. ***(Expressen)***

**AARONS AITAKA ENGLAND**

MLINZI wa pembeni wa Norwich City, Max Aarons mwenye umri wa miaka 21, amesema akili yake ni England na sasa hana mpango wowote wa kwenda kuichezea Jamaica nchi ya asili yake. ***(Norwich Evening News)***

## HABARI MICHEZO

# UKITAKA KUIPIGA YANGA KAMATA KISINDA - MALALE

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kufanikiwa kulazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha juzi, Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, ameanika mbinu za kuishika timu hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Malale alisema ndani ya kikosi cha Yanga, ukishamdhibiti winga Tuisila Kisinda, huo ndio unakuwa mwisho wa timu hiyo kufurukuta.

"Wakati tunarudi vyumbani niliwaambia wachezaji wakimbana Kisinda, Yanga haina uwezo wa kufunga kwa haraka walifuata maelekezo yangu hatimaye tukatoka sare," alisema Malale.

Alisema mchezo huo ulikuwa mgumu na kudai wamefurahi kupata pointi moja kwa kutoka kwa timu kubwa ambayo inaongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hata hivyo, alisema lengo lao ni kuendeleza ushindani na kushika nafasi za juu katika msimamo huo.

Akizungumzia uwepo wa mchezaji wake Kelvin Yondani kuwa ameongeza chachu ya ushindani katika kikosi chake, alisema nguvu yake inaonekana.

"Ni mchezaji ambaye akiwa uwanjani anajua kujituma pamoja na kufuata maelekezo aliyopewa na kocha," alisema.




Katibu Mkuu wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk. Kiagho Kilonzo, akizungumza na wadau wa filamu jana, jijini Dar es Salaam, wakati wa hafla fupi ya kutangaza rasmi fursa ya ufadhili wa filamu za Kitanzania zinazotolewa na kampuni ya MultiChoice kupitia kampuni yake tanzu ya M-Net. **MPIGAPICHA WETU**

# M-Net yatangaza neema kwa wazalishaji filamu Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

M-Net, Kampuni tanzu ya MultiChoice, ambayo kwa zaidi ya miaka 30 imejizolea umaarufu mkubwa kwa vipindi vyake vya burudani hususan filamu, imetangaza neema kwa tasnia ya filamu Tanzania ambapo imeanza kuitisha mapendekezo kutoka kwa wazalishaji kwa ajili ya ufadhili wa filamu za Kitanzania.

Kwa mujibu wa M-Net, sasa imeanza kupokea mapendekezo kutoka kwa wazalishaji wa filamu hapa nchini kwa ajili ya kufadhili uzalishaji wa filamu hizo ambazo zitatumiwa na M-Net kwenye chaneli zake sita zilizopo Afrika Mashariki zinazoonyeshwa katika kisimbuzi cha DStv.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu ufadhili huo, Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo, alisema kuanzia sasa hadi Machi 14, mwaka huu, M-Net itakuwa ikipokea mapendekezo kutoka kwa wazalishaji wa filamu za wa hapa nchini na hatimaye itayapitia kisha kuchagua filamu ambazo zitapata ufadhili huo.

"Kwa sasa M-Net imekuja na mpango mkubwa zaidi mahususi wenye lengo la kupata fiamu nyingi zaidi za Kitanzania na sasa wazalishaji wetu wanatakiwa wachangamkie fursa hii adhimu kwani kama mnavyofahamu, chaneli za M-Net zinazorushwa kupitia DStv huonekana katika nchi mbalimbali duniani.

"M-Net imeaua kufadhili filamu halisi za Kitanzania zinazoakisi mila na desturi za Kitanzania huku zikibeba maudhui mbalimbali ikiwamo maisha ya kila siku, mapenzi, mahusiano na kadhalika ilimradi tu yawe yanaakisi uhalisia na utamaduni wa Kitanzania," alisema Shelukindo.

Alisema filamu inatakiwa kuwa katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Kwa zile za Kiswahili, zitapaswa kuwa na tafsiri ya Kiingereza (subtitle) na kwamba. simulizi inatakiwa kuwa yakusisimua na kumfanya mtazamaji kuwa na hamu na shauku ya kusubiria awamu nyingine.

Shelukindo aliyataja mahitaji yanayopendekezwa kuwa ni pamoja na kulenga watazamaji wa umri kati ya miaka 20 hadi 45, muda- dakika 90 na iwe kwa Kiswahili au Kiingereza. Pia mzalishaji anapaswa kuwasilisha muongozo wa filamu, wasanii watakaocheza, majina kamili ya timu ya waandaaji, bajeti ya awali, sampuli ya kazi yoyote ya awali iliyofanywa na muombaji na pia stakabadhi ya kimkataba, ikielezea majina kamili ya kampuni, waongozaji, wadau, vielelezo vya usajili wa kampuni, hati za usajili Mamlaka ya Mapato (TRA) na anuani kamili.

Aidha, alisema wazalishaji wanaowasilisha mapendelezo yao wayawasilishe kwa njia ya barua pepe ambapo mwisho wa kupokea mapendekezo ni Machi 14, mwaka huu.

Serikali kupitia Bodi ya Filamu, imepongeza uamuzi huo wa M-Net na kuwataka wazalishaji wa filamu Kitanzania kuchangamkia fursa hiyo adhimu na kuhakikisha kuwa wanapeleka mapendekezo ya viwango vya juu kwani huu ni ulingo muhimu wa kutangaza na kupanua soko la tasnia hiyo.

Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk. Kiagho Kilonzo, amesema hii ni fursa kubwa na bodi yake imejipanga kushirikiana na mashirikisho yote ya filamu hapa nchini kuhakikisha kuwa wazalishaji wanaitumia fursa hiyo vizuri huku wakihakikisha haki na maslahi yao na wasanii yanazingatiwa.

## Daraja la Kwanza Z'bar mabao 178

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

JUMLA ya mabao 178 tayari yamefungwa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja inayoendelea visiwani Zanzibar.

Mabao hayo yametokana na mechi 76 zilizochezwa katika mzunguko wa kwanza na wa pili ambao umeanza wiki hii.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamo Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Zanzibar (ZBL), Sheha Mohmmed, alisema ligi hiyo hadi sasa inaendelea vizuri kama ilivyopangwa katika mzunguko huu wa lala salama.

Alisema tangu kuanza kwa mzunguko wa pili bodi hiyo haijapokea malalamiko yoyote kuhusu ratiba wakati huu ligi hiyo ikitarajiwa kumaliza Aririli 13, mwaka huu kama ilivyopangwa ili kupisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

**"Ligi inaendelea kuchezwa kama ilivyopangwa, mpaka sasa hatujapata malalamiko, timu zote zinafuata ratiba na muda uliopangwa wa kucheza mechi zao," alisema.**

## Ligi Kuu Zanzibar ubingwa hautabiriki

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa lala salama ikiendelea kupamba moto visiwani hapa, hakuna timu yoyote kati ya 12 zinazoshiriki kinyang'anyiro hicho, hadi sasa ambayo inaweza kujihakikishia nafasi ya kutwaa taji hilo msimu huu, takwimu zinaonyesha.

Maabaria wa KMKM ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 29, nafasi ya pili ikishikwa na KVZ yenye alama 26 na ya tatu ikikaliwa na Maafande wa Mafunzo wenye alama 24 huku timu zote zikiwa tayari zimeshuka dimbani mara 14.

Kwa upande wa timu zinazobura mkia ambapo msimu huu zitashuka daraja mbili, ni timu ya Maafande wa Polisi ikiwa na pointi 15 katika na nafsi ya 11 huku timu ya Hard Rock yenye alama 11 ikiendelea kusalia mkiani.

Wadau wa soka visiwani hapa, wametoa maoni yao wakieleza kuwa ligi hiyo inapoteza msisimko kutokana na kukosa udhamini.

Mmoja wa wadau hao, Massoud Mohmed, alisema: "Kama ligi hii ingekuwa na ufadhili ingekuwa nzuri zaidi kwakuwa timu zinajua zinacheza na mwisho wa msimu kipo wanachokipigania."

Michezo
Jumanne Machi 9, 2021
Nipashe



## FERNANDES AFUNGUKA MAZITO PENALTI

HABARI UK 22

MNAHESABU?...



Kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandes, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la kwanza kwa mkwaju wa penalti wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya mahasimu wao, Manchester City kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Etihad juzi. **PICHA: MTANDAO**

# NDAYIRAGIJE, MAXIME KATIKA MIZANI YANGA

●●●Mwambusi mapema tu, Kaze asema subira ni ngumu kwa watu wengine hivyo anaenda kujifua mbele...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kamati ya Utendaji ya Klabu ya Yanga, ikieleza kuwa inatarajia kukutana leo jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujadili na kuweka wazi juu ya mchakato wa kupata kocha mkuu atakayerithi mikoba ya Mrundi Cedric Kaze ambaye mkataba wake umevunjwa rasmi juzi usiku, aliyekuwa Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije na Mecky Maxime aliyetimuliwa Kagera Sugar, wapo katika mizani moja ya kuinoa.

Kaze alitimuliwa sambamba na benchi zima la ufundi kuvunjwa, uamuzi huo ukifikiwa baada ya Yanga kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha juzi, sababu ikiwa ni mwenendo mbovu wa matokeo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaze alisema amefurahi kwa miezi yote mitano ambayo ameifundisha Yanga na kuipa Kombe la Mapinduzi, lakini anachokiona ni subra kukosekana kwa watu wengine, hivyo hana budi kwenda kujifua mbele ya safari.

"Nimefurahi miezi mitano tuliyokuwa wote, tumetumika pamoja. Tumepata furaha na wakati mgumu, lakini hakuna jinsi ndivyo mpira ulivyo, subira ipo ngumu kwa watu wengine, naenda kujifua mbele. Nimewapati furaha na kwa miaka mitatu (bila kombe), nimewapatia kombe la kwanza ambalo ni la Mapinduzi," alisema Kaze.

Lakini wakati Kaze akieleza hayo, taarifa za ndani zilizolifikia Nipashe jana zinaeleza makocha ambao wapo katika 'mizani moja' ya kuinoa timu hiyo ni Ndayiragije na Maxime huku Juma Mwambusi yeye akitarajiwa kupewa mikoba hiyo mapema ili kuendelea kuwaweka sawa wachezaji.

"Unajua Mwambusi ambaye aliomba kupumzika ili kwenda kujiuguza, tayari anawafahamu vizuri wachezaji wote kikosini, hivyo itakuwa rahisi kwake kuwaunganisha na timu kuendelea kupata matokeo, lakini kuna kazi kubwa ya kumshawishi Maxime kukubali kuwa kocha msaidizi wa Ndayiragije.

"Kwa Mwambusi hana makuu ni mwelewa ndiyo maana awali alikubali kuwa msaidizi wa Kaze, hivyo ni rahisi kumshawishi kuwa msaidizi wa Ndayiragije kuliko Maxime," kilieleza chanzo chetu ndani ya uongozi wa timu hiyo. Nipashe lilipomtafuta Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa, kutaka kujua ukweli kuhusu makocha hao wanaotajwa, alisema hizo ni tetesi tu kwa sababu hawajatangaza jina la kocha yeyote ambaye atakuja kurithi mikoba ya Kaze.

Alisema baada ya juzi kutoa taarifa ya kuvunja benchi la ufundi, uongozi unatarajia kukutana leo, kwa ajili ya kuweka mambo sawa ikiwamo mchakato ambao utatumika kwa ajili ya kupata benchi zima la ufundi.

"Bado hatujaweka wazi, mchakato upi tutatumia kupata benchi la ufundi, kwa sababu tulitoa taarifa ya kuvunja benchi la ufundi tukiwa Arusha, sasa tunarejea nyumbani na kesho (leo), Kamati ya Utendaji itakutana kwa ajili ya kuangalia mchakato upi ambao tutautumia kupata benchi la ufundi," alisema Mfikirwa.

Alisema wanahitaji kufanya mchakato huo mapema ili benchi la ufundi litangazwe hivi karibuni kabla ya ligi kuendelea kushika kasi mzunguko wa pili, ambao kwa sasa itasimama kwa muda wa wiki tatu kupisha kalenda ya michuano ya kimataifa.

## SIMBA YAPANIA 6 KWA MERRIKH, AS VITA CAF

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuvuna pointi saba katika mzunguko wa kwanza wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wawakilishi wa nchi kwenye michuano hiyo, Simba, wametangaza vita ya kuhakikisha wanavuna pointi zote sita za mechi mbili za nyumbani dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan na AS Vita ya DR Congo.

Jumanne ijayo Simba itaikaribisha Al-Merrikh katika Uwanja wa Benjamin Mkapa huku Aprili 3 ikiikaribisha AS Vita kwenye dimba hilo kabla ya Aprili 10, mwaka huu kwenda ugenini nchini Misri kuhitimisha hatua hiyo ya makundi kwa kuivaa Al Ahly.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema wanahitaji kuchanga karata vizuri kwa ajili ya mechi zilizobaki husan za nyumbani ili kuvuna pointi zote sita na kufikia malengo yao.

> **"Tuna kazi kubwa ya kuhakikisha tunapata pointi sita za nyumbani ili kuendelea kujiimarisha katika nafasi tuliyopo kwa kuongeza pointi," alisema Gomes.**

Naye mshauri wa klabu hiyo, Crescentius Magori, alisema kwa sasa wachezaji wanatakiwa kupambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri kwa kutafuta pointi sita katika mechi mbili za nyumbani.

"Mechi yetu dhidi ya Al-Merrikh ilikuwa ngumu sana, pia sare ya Al Ahly dhidi ya AS Vita, inatupa mwanga kwamba tunahitaji kupambana kushinda mechi zetu za nyumbani, pia tuachane na ile dhana ya kwamba anayekuja Uwanja wa Benjamin Mkapa hatoki mtu," alisema Magori.

Simba inaongoza Kundi A ikiwa na pointi saba baada ya kuichapa AS Vita kwa bao 1-0 kwao na kisha kuibuka na ushindi kama huo hapa nyumbani dhidi ya Al Ahly kabla ya sare tasa nchini Sudan dhidi ya Al-Merrikh.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002